# *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*

Kwa Mwenyezi Mungu, iwe shukrani na sifa milele. Kwa kundi hili zuri la wahudumu ambao wamefanya kazi katika uamsho huu, ninataka kutoa shukrani zangu kwao kwa ajili ya moja la kundi zuri sana la watu niliopata kufanya kazi nao maishani mwangu. Kwa maskini mpiga kinanda mzuri hapa, na mpiga piano, kwenu ninyi nyote watu wapendwa, mabawabu, asilimia mia moja kutoka kwa watu walio bora sana, hata kwa shule hii kwa kuturuhusu kupachukua mahali hapa kwa ajili ya ibada, na kwa yote ambayo yamefanywa, kamwe sijui jinsi ya kujielezea katika shukrani kwa ajili ya mkutano huu. Ninaomba ya kwamba matokeo kutoka kwenye huu kamwe hayatakufa, bali yataendelea kuishi.

2 Ninasikitika sikuwa na wakati zaidi wa kukutana na watu hawa na kuwa makanisani mwao, na kadhalika. Walikuwa tu wakininukulia, dakika chache zilizopita, juu ya vijana kumjia Kristo asubuhi ya leo, nguvu za Mungu mikutanoni mwao. Ninatumaini hilo kamwe halitakufa bali litaendelea milele mpaka Yesu atakapokuja.

3 Wengi wenu marafiki wema ambao nimekutana nao tangu nimekuwa hapa, kumbukumbu zenu zitadumu moyoni mwangu: ushirikiano. Mahubiri magumu, makali yanayonibidi kufanya wakati mwingine. Mimi si ninii . . . Sidai kuwa ninii, tunachoita, mhubiri; mimi ni . . . Mnajua hilo tayari; bali ni—ninadai tu kumjua Bwana kama Mwokozi wangu, nina shauku sana nikijaribu ku—kufanya kile ambacho Yeye amechagua kifanywe; na kwa jambo hili Yeye amenipa nafasi, kwa karama, kuwaelezea watu, kwamba, ambapo sitakuwa na elimu kulifanya, labda zile kazi zitaonyesha kwamba mimi—mimi ni mtumishi Wake, na—nawe ni ndugu yangu na dada, na hilo litalithibitisha. Na labda hilo litawafanya kujua ya kwamba ninawapenda, Mungu anawapenda; na pamoja tunatumaini kutumia Umilele usio na mwisho pamoja katika Nchi iliyo ng'ambo ya mto, mahali fulani kule.

4 Juma lijalo, Jumapili ijayo, juma moja kuanzia Jumapili hii, kama nilivyotoa lile tamshi fidhuli, nitaanzia kwenye viunga vyenu sasa, juma lijalo kuanzia Jumapili hii ijayo. Hiyo ni Chicago (Mnaona?) hapa juu, viungani mwa mji huu. Na kwa hiyo sisi . . . kamwe sijui iko wapi; ni—ni Bwana . . . Kamwe siwezi kukumbuka jina hilo la Kiitalia, Bottazzi . . . Ati nini? Bottazzi. Ametangaza mahali ambapo ibada hizo zitafanyiwa

huko Chicago? Tayari imetangazwa kutoka jukwaani. Hata mimi sijui mahali zilipo. Na kwa hiyo tutapapata kwa njia fulani; nitafika kule na kumpigia simu Ndugu Carlson, mtu fulani, nipate kujua mahali ninapopaswa kuwa. Na kwa hiyo tunatarajia mambo makuu huko Chicago juma lijalo. Tungefurahia ukiwa mgeni we—wetu huko Chicago, na, ama mkutano mwingine wowote tungaliweza kuwako.

5 Sasa, wakati mmoja, nimesema usiku kamwe usingeweza kuwa na giza kupita kiasi, wala mvua isingeweza kunyesha kupita kiasi, ila ambapo ningekuja kwenu, kuwasaidia, kwa lolote ambalo ningeweza linalohusu Ufalme wa Mungu, ama jambo lingine lolote ambalo ningeweza kuwasaidia. Kama ningalikuwa na pesa kidogo, na kama mimi…na kama mlizihitaji, zingekuwa zenu. Hiyo ni kweli, ningefanya hilo. Mtu yeyote anayejua maisha yangu na familia yangu, ilikuwa ni vivyo hivyo. Maskini baba yangu mkongwe ametuacha leo; yeye hakuishi maisha yafaayo duniani. Alikuwa na tabia moja mbaya: kunywa pombe. Lakini kama angekutana na mtu mtaani, mgeni kabisa, naye huyo mtu alikuwa na njaa naye alikuwa na biskuti moja, yeye angeivunja vipande viwili amgawie. Tunaamini katika kuwasadia wahitaji; katika kusaidia.

6 Laiti ningaliweza kusema ningekuja kwenu wakati wowote. Ningetaka kusema hivyo, bali siwezi; wapo wengi kupita kiasi. Mkutano huu mdogo tu hapa, ambao ni kundi dogo tu la watu, sasa wazia ulimwengu mzima: mamilioni. Mnaona, nisingeweza kusema hilo kwa haki. Bali nitafanya hili, rafiki. Nitafanya yote niwezayo. Ikiwa—ikiwa unataka niombee leso kama hii hapa, nikutumie; iwapo huihitaji sasa nawe unaitaka haidhuru, agiza, uipate. Hakuna malipo juu ya chochote.

7 Hatulipishi chochote. Hakuna malipo kwa ajili ya huduma, hata kwa vitabu vyetu. Hivyo si vitabu vyangu. Ni vya watu mbalimbali walioviandika vitabu hivyo. Mimi huvinunua kwa asilimia arobaini chini. Nawapa mawakala wangu wa vitabu nao wana mamlaka ya maamuzi mlangoni: kama mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana akiingia, anataka moja ya vitabu hivyo, wala hana pesa za kukilipia, mpe haidhuru. Nasi sikuzote hupata hasara kwa hivyo vitabu. Hakuna njia ya kupata, yaani, kutopata hasara. Nayo ile picha ya Malaika wa Bwana: hiyo si mali yangu, hiyo ni mali ya Studio za Douglas, nayo imepewa haki ya kunakili wala isingeweza kutolewa tena, maana ungekuwa ukikiuka haki za kunakili.

8 Kwa hiyo si—si zetu. Nasi huzileta tu, kwa sababu tunafikiri zingemsaidia mtu fulani. Na kuvinunua vitabu hivyo kwa asilimia arobaini chini, halafu labda kupoteza asilimia kumi ama kumi na tano za hivyo kabla havijawafikia; kisha inakubidi kuwalipa wavulana hawa kuviuza hivi. Kanisa linawapa kiasi fulani kwa juma. Na jambo lingine, si vyangu; maskani ndiyo inayovishughulikia hivyo.

9 Na kila kitu tufanyacho ni bure. Sasa, sijaribu kupata anwani zenu. Mimi sininii. . . Kama ninavyosema, nina ninii. . . Vema, katibu wangu, yeye huifanya kazi yangu. Sijui kama. . . Uko hapa, Jim, leo? Sijui kama alifika huku ama la. (Baba mkwe wake yupo hapa, nafikiri, na mama mkwe wake, Bw. na Bibi Fred Sothmann.) Wapo hapa: mke wake ni. . . hujibu simu; Ndugu Jim hupiga chapa.

10 Ndugu Leo Mercier hufanya kazi ya nje. Alikuwa hapa dakika chache tu zilizopita; mwenzake hapa. Wao. . . wavulana hawa huifanyia kazi Maskani ya Branham, ambayo mimi ni mshiriki wake, ambalo ni kanisa huru linalojitawala, lililosajiliwa Jeffersonville katika Mkoa wa Clark. Na ni taasisi isiyoleta faida, nazo pesa zinazoingia kanisani na kadhalika, ni. . . zinaenda kwenye huduma za nchi za kigeni kuwadhamini maskini wasio na pesa za kutuma nipate kuja huko, lakini hata hivyo wananihitaji sana.

11 Na mimi huzichukua pesa hizo, mara wanapoweka akiba ya kutosha, na kwenda kwenye huduma za nchi za kigeni kuwahubiria hao, Injili ii hii mlio na majaliwa ya kuiona. Na kwa hiyo, ninajua kama msimamizi wa pesa Zake, itanibidi kuwajibika kwa ajili yake kwenye Siku ya Hukumu. Basi mimi huzichukua, mimi mwenyewe, mradi tu mimi ni mdogo kutosha kwenda, na ninaweza kwenda, ninataka kwenda kuhakikisha ya kwamba ninahubiri na kuwaletea Ujumbe ambao mlichangia wapate kuusikiliza. Hizo sifa njema zote na ziwe zenu kwenye Siku hiyo. Mimi ni mtumishi Wake tu wa kuubeba Ujumbe.

12 Nadhani, kama vile hawa wavulana, mmoja alivyosema muda mfupi uliopita, walichukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Hiyo haikuhitajika. Sikuja kwa ajili ya hiyo. Nimekuwa nikihubiri kwa muda wa miaka thelathini na mmoja. Nilichunga maskani ya Baptisti kwa miaka kumi na saba. Nendeni mkaangalie kwenye vitabu, kamwe sikuninii. . . mwulizeni mtu yeyote kote nchini mahali popote; kamwe sijachukua sadaka maishani mwangu mwote, kamwe, maishani mwangu mwote.

13 Wakati mmoja wakati nikifanya uchungaji maskanini, sisi kama watu maskini, tulipungukiwa kidogo na pesa. Sote tunajua hicho ni kitu gani, sivyo? Tulikuwa tu na madeni fulani tuliyopaswa kulipa, mimi na mke wangu, Billy alikuwa ni mchanga sana wakati huo. Ndipo ni—nikasema, “Unajua nitakalofanya? Ninaenda kuchukua sadaka usiku wa leo.” Hapo ndipo nilipokaribia sana kufanya hilo.

14 Basi ndugu mzee aliye Utukufuni leo hii, Ndugu Wiseheart. . . Hatukuwa na sahani ya sadaka; tulikuwa tukiliweka kwenye ma—magazeti mjini: “Kanisa lisilo na sahani ya sadaka.”

15 Nilifanya kazi, nikajitahidi, chochote ningaliweza kufanya kupata riziki. Nalo kanisa, sio kwa sababu wasingeweza

kunihudumia: Kama ningeweza kufanya kazi, kwa nini nisifanye kazi? Watu wengine walifanya kazi. Paulo alifanya kazi. Kwa nini isiwe mimi? Nayo sababu, ule uchovu mkubwa wa kazi mahali mahali, ama ningali, afadhali nije papa hapa na kuchukua zana za kazi na kwenda huko nje mtaani na kufanya kazi siku nzima, nije na kuwahubiria usiku. Hiyo ingekuwa ndiyo shauku yangu, kama ningaliweza kufanya hivyo. Hilo ni mbele za Mungu na Biblia yangu.

16 Lakini ilitubidi kupata pesa kidogo. Nilihitaji kama dola tano, nami nilikuwa nimetoa ahadi; na nilikuwa nina deni, ka—ka—kamwe sikuwa nazo. Wala tusingeweza kuzipata. Kwa hiyo nikasema, "Ninaenda, kuchukua sadaka usiku wa leo."

17 Maskini mke wangu mpendwa, kama kuna sifa yoyote njema inayoiendea familia ya Branham, na imwendee yeye. Yeye ndiye aliyesimama kati yangu na umma katika mambo yote ambayo yamefanywa, mwacheni yeye apate sifa. Ananiambia, "Billy, nitaenda nikuone ukifanya hilo."

18 Nikasimama usiku huo. Yeye alikuwa ameketi nyuma; nikasema, "Marafiki, nimekuwa nikifanya uchungaji hapa, nadhani, yapata miaka kumi na miwili." Nikasema, "Kamwe sijawahi kuchukua sadaka; Nina haja kidogo tu usiku wa leo, kweli nahitaji kama dola tano." Nikasema, "Mimi... Kama mimi...Tutapitisha kofia huku, kama una nikeli moja ama mbili, ungeweza kuweka..." Kusanyiko langu liko hapa limeketi humu sakafuni papa hapa. Nikasema, "Kama ukitaka, una nikeli ama senti ungetaka kunisaidia nayo, ningelithamini sana." Hatukuwa na sahani ya sadaka; nikasema, "Ndugu Wiseheart, waweza kuichukua kofia yangu?"

19 Ikatokea niliangalia pale chini, na maskini mwanamke mmoja, yuko Utukufuni leo hii; jina lake lilikuwa Bibi Weber. Alikuwa amevaa moja ya aproni hizi ndo—ndogo, zilizo na mfuko chini ya hiyo aproni. Ninyi wanawake mliwahi kuona moja ya hizo? Nadhani mama zenu walizivaa miaka mingi iliyopita. Aliingiza mkono mle na kushika moja ya vitabu hivi vidogo vilivyo na kibanio kidogo juu yake, mwajua, una... Ilikuwa ni katika nyakati ngumu sasa; hiyo imekuwa ni kama miaka ishirini na mitano iliyopita. Akakifungua kitabu hicho kidogo; akaanza kupapasa-papasa hizo nikeli. Nisingeweza kuichukua. Ni—nisingeweza kufanya hivyo, hapakuwapo na lingine. Ni—ni—nikaangalia pale chini, nami nikawazia, "Loo, rehema."

20 "Loo," nikasema, "Nilikuwa nikiwatania tu; nilitaka tu kuona kile mngesema. Nilikuwa tu nikiwachezea." Ndugu Wiseheart alikuwa na kofia yangu mkononi mwake; "Loo," nikasema, "Ndugu Wiseheart, itundike kofia yangu juu. Nilikuwa tu nikilitania kanisa."

21 Na kwa hiyo nikaenda nyumbani nami nikawazia, “Vema,” nikashuka, duka la bei rahisi, ndipo nikanunua kopo la rangi la senti kumi. Yupo mzee ambaye ameenda Utukufuni sasa. Ndugu Gene, mnamkumbuka vizuri, mzee Ndugu Ryan. Alikuwa na nywele ndefu, na ndevu ndefu, yeye aliiendesha baiskeli hii kule chini, naye akanipa. I—ilimrudia nyuma na . . . La, hilo si zuri kwa Mbaptisti kusema, sivyo? Hebu tuseme tu ilichakaa, ilichakaa tu. Na sasa mimi ni Mbaptisti; mimi ni Mbaptisti Mpentekoste (Mnaona?), mmoja wa . . .?. . . Mbaptisti aliye—aliye na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo nikasema . . . nikaenda kule na kuichukua baiskeli hii chakavu nikashuka na kujinunulia kopo la rangi, nikaipaka rangi na kuifanya ionekane nzuri kweli, nikaipiga msasa, na kuiweka upande wa mbele, nikaiuza kwa dola tano. Kamwe haikunibidi kuchukua sadaka hata hivyo. Kwa hiyo hapo ndipo nilipolikaribia sana.

22 Asanteni, rafiki zangu, kwa yale yaliyokuwa kwenye hayo matoleo. Yataenda kwenye hazina, na kutoka hapo yataenda kwenye huduma za nchi za kigeni kuuleta Ujumbe huu kwa makafiri na wale watu wasio na mlo mmoja, labda wa kula mara moja kwa juma. Huko ndiko yatakakoenda. Basi Mungu wa Mbinguni na awarudishie mara mia moja na kuweka matofali ya dhahabu katika yale makazi yenu ng’ambo ya anga, ndilo ombi langu.

23 Niandikieni wakati wowote sasa mtakao. Nipigieni simu. Mara nyingi kidogo siko huko Jeff sana. Anwani yangu: Jeffersonville, Indiana, Sanduku la Posta 325. Kama huwezi kukumbuka 3-2-5, itume tu, Jeffersonville.

24 Na endapo unataka kunipigia simu, namba yangu ni BUtler 2-1519. Usipoweza kuipata kwenye namba hiyo, basi piga BUtler 2-3826. Usipoipata kwa hiyo, piga BUtler 3-6771, usipoitapa kwa hiyo, loo, afadhali uachie hapo, kwa hiyo . . . Lakini kwa vyovyote vile namba maalum ya kunipigia unipate: BUtler 2-1519; hiyo ni kumi na tano kumi na tisa. [Namba za simu zimebadilishwa—Mh.] Hiyo ni ofisi, nao wanaweza kukwambia mahali ningeweza kupatikana. Saa yoyote ya usiku ama chochote ninachoweza kufanya kuwaombea kwa simu, kuwatumia kitambaa cha maombi ama chochote kile, bure kabisa, hakuna kitu, mnaona, ningefurahia kufanya hivyo.

25 Na sasa, nadhani, kuna mambo yamekuwa yakitukia kwenye mikutano yangu mitatu ya mwisho ambayo yamenishtusha sana. Asubuhi ya leo niliketi na mwanangu kwa karibu saa moja nami nikasema, “Billy, kuna shida gani?” Jana usiku, liliibuka tena: ninaondoka hudumani.

26 Kuna shida gani? Je, ninaenda Nyumbani? Kwani kazi yangu imekwisha? Hivi ninii yangu . . . huduma ya aina hii imemalizika? Ninaenda kwenye nchi za kigeni? Sijui mimi. Ninayasema mambo hayo, bali jambo fulani linakaribia kutukia. Sijui ni kitu

gani. Kwa hiyo kama ni kwenye eneo lililo ng'ambo ya mto huko, huko kwa wapagani, popote pale, ninajisikia kwamba Marekani imepata ujumbe wake. Na kama ndivyo, ninataka kuwaomba fadhila: Mpaka tutakapokutana tena kwenye ule mto mkubwa huko ng'ambo mwishoni mwa safari, mtaniombea? Asanteni.

27 Wakati mchawi anaponipa changamoto ya mjadala, wakati pepo wa kila namna kwenye maeneo ya nchi za kigeni, kama nitaitwa, kama vile wanavyofanya kwa kawaida, nitakumbuka huku katika Bloomington, Illinois, na miji jirani, ninalo kundi la watu Jumapili alasiri walioinua mikono yao, "Nitakuwa nikikuombea." Na wakati inaponibidi kutembea sakafuni kukabiliana nalo, nitajua ya kwamba nimefunikwa na Damu katika maombi yenu.

Tunaweza kuviinamisha vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi?

28 Baba mwenye rehema, tunatoa shukrani Kwako kutoka kwenye kilindi cha nafsi yetu kwa yote ambayo tumesikia kutoka Kwako, tumesoma kutoka kwenye Neno Lako, na kukuona Wewe ukitudhihirishia juma hili. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya watu hawa wazuri, kwa ajili ya wahudumu hawa wazuri, kwa ajili ya makanisa yao mazuri, kwa ajili ya chuo hiki mashuhuri, kwa ajili ya jumba hili la mikutano, kwa yote ambayo yamefanywa na kusemwa, kwa mabawabu, kwa wacheza muziki, kwa waimbaji, kila kitu tu, Baba. Kama nikiwakosa wowote, wabariki, Baba.

29 Umeona kila hatua ndogo, kila hatua ndogo ya neema. Umemwona mama, baba, wakiweka sehemu ya riziki yao kuusaidia mkutano huu. Walifanya hivyo kwa sababu Wewe ulikuwa ukizungumza nao. Tusingeweza kuwarudishia, wala tusingewarudishia, kwa kuwa tungewanyang'anya baraka zilizowekwa ng'ambo kidogo tu. Kwa kuwa siku moja tunasoma katika Biblia ambapo Yesu alikuwa akiangalia, matajiri wakiweka pesa nyingi katika sadaka, lakini maskini mjane mmoja akaja hapo na kuweka kama mapeni matatu. Bwana, nadhani, kama ningalikuwa nimesimama pale, ningalikimbia na kumshika mkono, niseme, "Usifanye hivyo, dada. Tunazo za kutosha humu." Bali Wewe ulikuwa umesimama pale, wala hukumzuia. Kwa kuwa ulijua kilichowekwa mbele kidogo. Ulijua ungemrudishia mara mia moja.

30 Kwa hiyo, Baba, ninajua ya kwamba Wewe, jicho Lako kuu, liliangalia kila hatua tuliyochukua. Tunaomba ya kwamba lolote tulilofanya, na jitihada dhaifu tulizokuwa nazo, kwamba imekuwa ikipendeza machoni Pako.

31 Ninatambua, Baba, ya kwamba ninawazungumzia alasiri ya leo wanaume na wanawake ambao, labda, kamwe sitawaona tena katika maisha haya. Wengi waliozeeka wameketi hapa na wagonjwa wengi. Siku moja ninatumainia kukutana nao huko

mtoni wakati wamebadilishwa kutoka kwenye maisha haya, kama vijana wanaume na wanawake waliooshwa katika Damu ya Mwana-kondoo, pamoja na miili ambayo kamwe haitakuwa na ibada nyingine ya uponyaji, wala hapatakuwapo na mwenye dhambi mwingine akililia madhabahuni. Ninaomba ya kwamba utawabariki.

32 Bariki wahudumu hawa, wachungaji hawa Wako, ambao katikati ya ukosoaji, wakati, Baba, kwa sababu ya msimamo wao wa kweli kwa Neno, jina langu si zuri sana miongoni mwao bali hawakuona aibu, waliniita kwa vyovyote vile. Ee Mungu, ibariki huduma yao. Jalia watambue ya kwamba mambo haya ni ya kulirejesha tu Kanisa kwenye msimamo wake ulio bora, kututikisa tu turudi, Bwana, kwenye mahali ambapo Roho Mtakatifu anaweza kujenga juu ya msingi halisi wa kweli, juu ya wanaume na wanawake halisi waliozaliwa mara ya pili. Baba, si kwa sababu sipendi mashirika yao, madhehebu, ni kwa sababu ninaona hiyo mifumo inawaacha watu walegee kupita kiasi. Tusaidie, Mungu. Unaujua moyo wangu, jinsi ninavyowapenda.

33 Ninaomba ya kwamba Wewe utatubariki pamoja tunapoligeukia Neno Lako sasa kwa ajili ya usomaji wa mwisho, kufungwa kwa uamsho huu, jalia, ama, sio uamsho huu, Bwana, siku hizi nane za jitihada; bali jalia uamsho kamwe usifungwe, jalia uzidi kuendelea zaidi na zaidi. Jalia udumu hata matokeo yangali yatakuwa hapa wakati Yesu atakapokuja. Kwa kuwa ninaomba ya kwamba Wewe utafanya jambo fulani alasiri ya leo litakaloyafunika yote, litakalowafanya watu kulisikia Neno kwa njia fulani hata Roho Mtakatifu ataipanda ile Mbegu kwenye kilindi cha moyo wao.

34 Moyo wangu ungali unamwendea maskini yule msichana mdogo niliyekutana naye pale mlangoni dakika chache zilizopita, ameketi amepindapinda kwenye kile kiti cha magurudumu. Jinsi ambavyo Wewe ulishuka kasi na kumwambia jinsi alivyofanyika hivyo, kile alichokuwa alipokuwa msichana mdogo, na kumwambia sababu ya yeye kutokuwa mzima, akitembea huku na huku sasa. Mungu jalia hilo lisiondoke moyoni mwa mtoto huyo. Yeye alipiga chapa barua ya kunialika. Ninaomba, Mungu, ya kwamba mtoto huyo atapona. Lijalie. Jalia lisiondoke kwenye maskini moyo wake, na ajue kwamba huyo aliyesimama pale hakuwa ni mimi, huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu akizungumza kupitia kwa mtumishi Wako, akimwambia yaliyo kweli kabisa, kile alichokuwa, kile alicho, na kile anachoweza kuwa. Jalia kamwe lisimwache, Bwana.

35 Bariki wote walio wagonjwa na wanaoteseka alasiri ya leo. Wakati watumishi Wako wanaposimama nasi tukiwaombea wagonjwa, jalia wote waponywe; jalia waliopotea waokoke, na Mungu apokee utukufu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

36 Mwombeeni Ndugu Roberts, Billy Graham, Tommy Osborn, Tommy Hicks, watu mashuhuri wa Mungu huko nje hudumani leo hii. Waombeeni. Sivyo? Ninyi waombeeni ndugu hao. Wanapiga vita vikali. Moyo wangu unawahurumia sana. Ombeni kwamba watadumu wakweli kwa Injili, na wakati yote yatakapokwisha sote tutakusanyika kama familia moja kubwa.

37 Hivi tuna vitabu vingine vilivyosalia kutoka kwa Wafanyabiashara kuhusu lile ono? Vyote vimekwisha. Kama wewe, mtu yeyote hapa ambaye hakupata nakala, inua mkono wako, hukupata nakala? wachache. Na—nadhani ya kwamba endapo ungeliandikia tu *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo, Los Angeles, wataninii. . .labda wana elfu chache zake zilizosalia. Wangefurahia kukutumia moja bure. Nadhani kama kuna—kama kuna malipo, yatakuwa ni senti moja ama kitu fulani. Sijui, kitu fulani tu kwa ajili ya gharama ya uchapishaji.

38 Kina lile ono, nami ninawatakeni mkisome. Basi mbele ya Biblia hii iliyofunguliwa, mbele za Mungu wangu, ninapaswa kujua maono yana maana gani. Hilo halikuwa ni ono. Nilikuwako kule. Niliiona. Sitaki kuninii. . .Ninachukia kusema hilo, kwa sababu mtu fulani anafikiri unajaribu kumwiga Paulo Mtakatifu mkuu. Sisemi hilo kwa ajili hiyo. Ninasema tu, ya kwamba ninajua Mahali fulani ng'ambo tu ya hapa kunayo Nchi tunakoishi tena. Kamwe ningewezaje. . .

39 Nilisema, nilipokuwa nikirudi, "Jalia nifanye yote niwezayo." Siwezi ku-. . .Siwajibiki kwa yale wasemayo wengine. Sina budi kuwajibika kwa yale nisemayo. Sijui yale. . .

Huenda ukasema, "Nimewasikia watu wakisema hilo. Na—natumaini ya kwamba kila sehemu yake ilikuwa ni kweli. Ninatumaini kwamba kila sehemu ilikuwa ni kweli."

40 Ndugu, dada, mbele za Mungu, hii ilikuwa ni kweli. Ilikuwa ni kweli. Ni—nilikuwa tu kama nilivyo sasa, ila tu kijana mwanamume tena, nikisimama Mahali fulani nikiwaangalia watu waliotoka ambako wazee walikuwa wamebadilika wakawa vijana, wala hapakuwapo na maradhi, hakuna huzuni, hakuna mauti. Walikuwa tofauti. Na hata hivyo, Yeye aliniambia yaliyo makuu kuliko hayo bado yanakuja. Hilo lingekuwa ni zuri kutosha kwangu kwa nyakati zote.

41 Nimewazia alasiri ya leo. . .Kunradhi; sitaki kuwa mtoto mchanga. Lakini unapokutana na watu, kisha unajua inakubidi kuwaacha, na labda, wajua, wazee namna hii, kama nikirudi mwaka mmoja tangu sasa, labda kamwe sitawaona tena. Nalo linanifanyia tu jambo fulani.

42 Lakini hebu tujaribu kufungua sasa. . .kwenye Mwanzo mlango wa 22. Nami ninataka kusoma sehemu tu ya kifungu cha 14, ama, kuwanukulia.

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yohova-yire: kama watu wasemavyo* hata *leo, katika mlima wa* B*WANA* *itapatikana.*

43 Mwanzo 14:22, ama, Mwanzo 22:14, samahani. Sasa, ninataka tu mnipe ninii . . . usikivu wenu sana wakati tu nikifundisha hili. Nami nitaharakisha; nina maili mia tatu katika dhoruba hii kuendesha gari alasiri ya leo nipate kutimiza matakwa ya kesho.

44 Kwa hiyo sasa, mimi . . . Lakini ninawatakeni mwe na hakika kujaribu kulishika, kumalizia yale niliyosema juma hili, juu ya kukaribia kwa Kuja kwa Bwana. Na sasa, endapo una penseli na karatasi, nina yapata Maandiko ishirini yaliyoandikwa hapa endapo mngetaka kuyarejea Hayo tunapoendelea kusoma, na kuandika muhtasari kidogo. Kwa sababu kwa kweli nafikiri ya kwamba hili ndilo jambo la wakati unaofaa sana ambalo Roho Mtakatifu amepata kuniruhusu kuzungumzia. Nami ni—ninatumainia ya kwamba katika kufanya jambo hili ya kwamba mtaelewa ya kwamba ni—ninaweza tu kulizungumzia; itambidi Roho Mtakatifu kulifasiri.

45 Sasa, nilizungumzia hili mara mbili tayari, na hii ndiyo mara ya tatu kuuendea ujumbe uu huu, kwa sababu ni wakati mzuri sana. Nami ninauita huu . . . Na kama mkiukosa, utakuwa kwenye kanda. Iwapo una kinasasauti cha kanda, mbona, hawa wavulana watawatumia kanda. Na sasa, waandikieni tu. Nadhani wao . . . mnajua anwani yao na kadhalika. Iwapo hujui, mbona, niandikieni tu mimi kule, nayo itapelekwa kwenye sanduku lao. Na wao ni wakfu wao wenyewe; wao ni Misheni ya Sauti huko Jeffersonville, na wavulana wawili wazuri, Bw. Mercier na Bw. Goad.

46 Nami nadhani mmeisikia hadithi yao jinsi walivyofanyika washirika wangu, ilikuwa ni kwa sababu walikuja kule kujaribu kunifichua, wakajifanya wenyewe FBI ndogo. Walikuwa wakija kule wala hawakuwazia ya kwamba hayo . . . hayo maono yalikuwa ni ya kweli. Ndipo wakaja kule wakipeleleza, na kujifanya kana kwamba walikuwa ni wahudumu, ndipo Roho Mtakatifu akayafichua maisha yao papo hapo mbele zao. Kwa hiyo wamekuwa washirika wangu. Mmoja wao Mkatoliki, Mfaransa Mkatoliki, Bw. Mercier, kabla tu ya uongofu wake alikuwa ni mtumishi wa baa. Bw. Goad anayeketi hapa, ninaamini, hapo awali, alikuwa ni . . . kutoka kwa watu waliotoka kwenye kanisa la Methodisti, si walikuwa watu wako? Mnazarayo aliyerudi nyuma.

47 Ulikuwa, ulifanya tu kazi katika ofisi mahali fulani, sivyo, Ndugu Goad? huko—huko Gary, Indiana. Mtumishi wa baa na mvulana wa ofisi, Mnazarayo aliyerudi nyuma na Mka- . . . wa Kirumi na Mfaransa Mkatoliki Mkanada, wakiwa pamoja kunifichua.

48 Nami ningeninii...Kama ninafanya jambo lolote baya, ninataka kufichuliwa. Na—na—na—na—nataka liwe sahihi, sasa. Huu ndio wakati wa kulirekebisha, sio nikisha kufika Kule. Hebu tulirekebishe, sasa.

49 Niliwabaini kuwa ni waungwana kweli, waaminifu, wavulana halisi. Wakati waliponiuliza kama wangeweza kutengeneza kanda...Inawabidi kujipatia riziki. Bw. Mercier ameoa sasa. Bw. Goad anajiandaa. Kukiwako na wasichana wowote ambao...Iwapo uso wake si mwekundu sasa!

Gene, nilifanya hivyo tu ili liwe ni kubadilisha kutoka... kujiandaa nipate kurejea kwenye somo hili.

Nitashuhudia yeye ni mtu mzuri. Yeye ni rafiki msiri wangu, ndugu halisi.

50 Na sasa, ni—nitauita huu, *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*. Nami ninataka kufikia upeo kwenye—kwenye Mwanzo 22:14, na Yehova-yire. Sasa, tunajua ya kwamba Mungu anayo Majina saba ambatani ya ukombozi. Sote tunafahamu hilo. *Yehova-yire* linamanisha, "Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu."

51 *Yehova-rafa* ni "Yehova, Bwana Mponya wetu"; *Yehova-manase*, "Bendera yetu"; Kinga yetu; Ngao yetu; *Kadhalika* yetu; kwenye: Majina saba ambatani ya ukombozi ni ya Yehova. Nalo Jina Lake la kwanza ni *Yehova-yire*, "Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu."

52 Sasa, sikilizeni kwa makini. Na ikikulazimu, jifanye tu mwenyewe, endapo mtu fulani ananong'onezea karibu nawe, sema, "Naomba unyamaze kwa dakika moja tu, tafadhali, kusudi nipate hili, unaona?" Ndipo watafanya hivyo. Watakuwa wazuri.

53 Sasa, tutaanza huko nyuma, turudi kule nyuma kabisa, tukiisha kufika hapa ambapo ninataka kuleta somo kwenye upeo, hebu turudi kwenye Mwanzo mlango wa 12. Kama ukitaka kuandika sehemu hizi, Mwanzo mlango wa 12.

54 Na sasa, tunaenda kuzungumza kuhusu Ibrahimu. Sasa kumbukeni, ya kwamba Ibrahimu...ile ahadi ilitolewa kwa Ibrahimu. Sote tunafahamu hilo. Hiyo ni kweli, ndugu yangu kasisi? Ahadi ilikuwa Ibrahimu, kwake.

55 Naye Ibrahimu hakuwa Myahudi. Ibrahimu alikuwa Mmataifa. Alishuka kutoka kwenye ule mnara, kutoka Babeli pamoja na baba yake, naye akaishi katika nchi ya Shinari kule, yale mabonde, na—na kuishi katika mji wa Uru, nchi ya Wakaldayo. Naye...Wa—Wakaldayo waliishi kwenye nchi hiyo, naye alikuwa katika mji wa Uru, na labda, mkulima. Naye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano kabla Mungu kumwita. Alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, nalo jina lake lilikuwa ni Sarai; jina lake lilikuwa Abramu; nao

walikuwa ni watu wawili wa kawaida tu. Basi siku moja Mungu akamwita Ibrahimu na kufanya agano pamoja na Ibrahimu (Sasa, angalieni.) na uzao wake baada yake.

56 Sasa, nitaweka vitabu viwili *hapa* na kuviita vitabu hivi (Mnaona?) kwa Ibrahimu na uzao wake baada yake. Sasa, yale aliyomtendea Ibrahimu, Yeye aliufanyia uzao wake baada yake. Wote wanaofahamu hilo dhahiri sasa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa Ibrahimu na uzao wake baada yake.

57 Sasa, kama tutaona katika Mwanzo 12 kwamba Mungu alimwita Ibrahimu kwa uteuzi, sio kwa sababu Ibrahimu alikuwa amefanya lolote kustahili hilo, si zaidi . . . Huenda alikuwa ni mwabudu sanamu. Sijui mimi.

58 Na Babeli, wanaabudu mizizi na . . . Kama ulipata kukisoma *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, ile historia ya kale, ungeona kwamba Babeli, iliyoanzishwa na Nimrodi: ilikuwa ni ibada za sanamu kikamilifu, hivyo tu. Naye alikuwa ni . . . Tunaiona Babeli mwanzoni mwa Biblia, katikati ya Biblia, na mwishoni mwa Biblia. Nayo ilikuwa ni m—mfumo wa kimadhehebu. Babeli ulikuwa ni mji mkubwa ulioifanya miji mingine yote midogo kulipa kodi kwake (Mnaona?), kitu kama ma—makao makuu mahali fulani na ambako amri zilitolewa na hiyo mingine yote ililazimika kulipia mahali hapo pamoja. Naye Ibrahimu alikuwa ameshuka kutoka kule pamoja na baba yake. Sasa, Mungu alimwita kwa uteuzi.

59 Sasa, ndugu, ndugu zangu wapendwa wa thamani, kama ikitokea nikiuke utaratibu katika fundisho la Kimaandiko, mtanisamehe kwa ajili yake na mjue ni ujinga wangu? Mtafanya hivyo, tafadhalini? Na ndugu zangu wa kithiolojia huko nje, kama mkijisikia ya kwamba mimi . . . fundisho langu ni baya, mtalisahau tu? Mnaona, ninii tu . . .

60 Sasa, wengi wenu watu mnaniandikia barua mkisema, "Ndugu Branham, inatupasa kufanya *hivi* na kufanya *vile*?"

61 Sikuzote mimi husema, "Mwulize mchungaji wako." Mnaona? Kwa sababu nitafanya lolote niwezalo, kuwajibu juu ya mafundisho makuu ya kimsingi ya kiinjilisti ya Biblia. Lakini inapofikia kuhusu: "Inatupasa kufanya *hivi* na kufanya *vile*." Sikuzote ninawarejesha kwa mchungaji wenu, kwa sababu huenda tukaninii . . . Kila mtu, hakuna wawili hapa, ila ambao wasingekubaliana mmoja na mwingine katika mambo madogo madogo ya mazoea, kama inatupasa kuchanua nywele zetu kulia ama kushoto. Na yangu, sina shida na hilo. Kwa hiyo—kwa hiyo . . . Bali mnajua ninalomaanisha. Tu—tunayo mambo hayo, kwa hiyo daima mimi huliambia tu kila kusanyiko, "Mwulizeni mchungaji wenu mambo hayo." Kama yeye amewaongoza umbali wa kutosha kuokoka na kujazwa na Roho Mtakaifu,

hivi hamwezi kumwaminia safari iliyosalia? kama Mungu alimheshimu kwa ajili ya jambo hilo.

62 Lakini juu ya kulileta wazo hili la wakati unaofaa kwa watu alasiri ya leo, itanibidi kutumia fundisho kidogo tu, ambalo linaweza kuingizwa, ama, kitu kama hicho, bali endapo hufikiri kwamba ni sawa, liweke tu kando na uendelee. Kama mchungaji akifundisha lolote tofauti kidogo, sahau niliyosema kulihusu (Unaona?), kwa sababu ninajaribu kufikia jambo muhimu. Natumaini hilo ni sawa. Natumaini hilo limefanywa dhahiri.

63 Lakini, mnaona, Ibrahimu mwenyewe akiwa si kitu, yeye ali—yeye aliitwa kwa uteuzi. Basi ikiwa Ibrahimu aliitwa kwa uteuzi, basi uzao wake baada yake hauna budi kuitwa kwa uteuzi. Hiyo ni kweli.

64 Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Hiyo ndiyo sababu unaihubiri tu Injili kwa urahisi wake; hata hivyo kondoo walioteuliwa wa Mungu wataisikia hiyo, na kuishika upesi sana, nao watauamini ubatizo huo wa Roho Mtakatifu (ambapo wengine wataondoka na kuudhihaki) kwa sababu waliteuliwa wapate kuusikia. Hivyo tu, mnaona?

65 Kwa hiyo mnaona sasa, ni kwa nini Kanisa, lenyewe, limeteuliwa. . . liliteuliwa na Mungu tangu zamani. Sasa, hebu nichukue Neno kutoka kwa Wathesalonike wa Kwanza m—mlango wa kwanza pale ambapo lilisema, "Kuchaguliwa tangu zamani." Sasa hilo si neno zuri kutumia mbele ya watu, kwa maana kuchaguliwa tangu zamani ni. . . Lingekuwa afadhali kama tungalilitumia hivi: kwamba ilikuwa ni kwa kujua tangu zamani, Mungu kwa kujua Kwake tangu zamani angeweza kuchagua tangu zamani kwa utukufu Wake Mwenyewe. Mnaona?

66 Yeye—Yeye hakusema, "Sasa, nitakuchagua *wewe*. Na nitakupeleka *wewe* jehanamu. Na nitakuchagua *wewe*, na kukupeleka *wewe* jehanamu." Hilo halikuwa ni wazo la Mungu. Yeye alitaka sisi sote tuje Mbinguni. Bali akiwa ni Mungu, Yeye alitangulia kujua ni nani angekuja, na ni nani asingekuja. Sasa, hilo linafanya dhahiri Warumi 4. . . Warumi 9, katika 8 na 9 pale, ambapo Yeye alisema ya kwamba ili lisimame imara kusudi la Mungu la kuchagua, kwamba kabla hajazaliwa mmoja wa wavulana hao, likizungumza juu ya Esau na Yakobo, Mungu alisema, "Nampenda Yakobo na kumchukia Esau." Mnaona? Kujua Kwake tangu zamani kulimwezesha kujua ya kwamba ninii yao. . . ya kwamba Esau hakuwa kitu ila tu ni ma—maskini laghai hata hivyo. Na kwamba Yakobo alikuwa na malipo kwa hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Kwa hiyo mnaona, kujua Kwake tangu zamani humfanya ajue. Kama Yeye hakujua

mwisho tangu mwanzo, basi Yeye hakuwa ni Mungu. Mnaona? Nayo Biblia ilisema ya kwamba sisi, kanisa . . .

67 Sasa, ninawatakeni mkumbuke: kunayo matabaka matatu ya watu, matabaka matatu ya watu duniani, yamekuwako sikuzote, na yatakuwako hadi mwisho. Sasa, hebu tuseme hilo pamoja: "Matabaka matatu ya watu: wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio." Liwekeni hilo akilini: matabaka matatu ya watu.

68 Sasa, sasa, tabaka lililoteuliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na wakaitwa katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Kristo alikuwa Mwana-kondoo wa Mungu aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Vema, Yeye alichinjwaje? Katika mpango mkuu wa Mungu Yeye alijua ya kwamba ange— angemtoa Mwana, naye huyo Mwana angekuwa ndiye Mwokozi wa watu Wake. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo Mungu anaponena jambo, limekwisha tayari. Loo, ndugu. Ikiwa . . .

69 Yu wapi maskini yule dada niliyekuwa naye, ambaye ono lilikuwa juu yake, dakika chache zilizopita? ameketi papa hapa kwenye kiti cha magurudumu. Kama ungeweza kuona hilo, dada mpendwa, yangekwisha kwako. Unaona?

70 Mungu anaponena lolote, Mungu anapotoa tamshi, ni la almuradi Yeye anasema hivyo, ni kamilifu, halina budi kutimia. Halina budi tu kutimia. Halafu basi Neno Lake linapoingia ndani yetu, haidhuru tunafanya nini, jinsi tunavyoonekana, tunalowazia, halina budi kutimia. Mnaona?

71 Kwa hiyo Mungu haiendeshi shughuli Yake . . . Kama Yeye alituokoa hapa, naye anajua atatupoteza baada ya kitambo kidogo, Yeye, mfanyabiashara duni. Na kwa hiyo basi wote aliowajua tangu zamani Yeye (nini?) amewaita. Wote ambao amewaita, amewahesabia haki; wote ambao amewahesabia haki, tayari amewatukuza. Sasa, kutakuwako na Kanisa litakalomlaki kule bila waa wala kunyanzi.

72 "Ndugu Branham, uko ndani yake?" Natumaini hivyo. Uh-huh. Lakini tunatimiza wokovu wetu wenyewe kwa hofu na kutetemeka. Na wakati unapoyaona maisha yako hayaambatani na Neno la Mungu, haidhuru wewe ni wa kanisa lipi, unajua uko nje ya utaratibu. Unaona? Basi endapo utafanya tu ninii yako . . . Ukifanya dini yako kwa sababu unajua ni jambo unalopaswa kufanya, unatumikia tu sehemu ya mnafiki. Iwapo humpendi Mungu kutoka moyoni mwako, basi wewe kwanza uko makosani. Unaona? Unapenda; upendo ndio unaodhibiti jambo hilo lote.

73 Sasa, sasa angalia. Ibrahimu aliitwa kwa uteuzi, si lolote alilofanya Ibrahimu. Basi angalia sasa, lile agano katika Mwanzo 12 (Mnaona?), agano lote lilitolewa kwa Ibrahimu; agano lote ni neema tupu (Mnaona?), sio "Ibrahimu, kama

utafanya jambo fulani, Mimi nitafanya jambo fulani." Haikuwa, "Kama—kama utafanya *hivi*, nitafanya *hivi*."

74 Mungu hufanya agano na mwanadamu, naye mwanadamu sikuzote huvunja agano Lake. Yeye alimwambia Adamu, "Ikiwa hutakula kutoka kwenye mti huo, utaishi," lakini Adamu akala kutoka kwake. Naye akamwambia lile agano alilofanya nao kwenye lile agano la Musa nyikani kule; walilivunja.

75 Kila wakati Mungu anapofanya agano na mwanadamu, mwanadamu hulivunja. Lakini wakati huu Mungu alifanya agano pamoja na Ibrahimu na uzao wake pasipo masharti. Sasa, mnaelewa? Sio, Ibrahimu, "Kama utafanya *hivi*, Mimi nitafanya *hivi*." Lakini, "Ibrahimu, nimelifanya tayari. Tayari nimefanya. . . Utakuja Kwangu. Umeokoka tayari; utakuja Kwangu katika umri wa uzeeni." Amelifanya tayari. Na sasa, sio leo, "Kama utafanya jambo fulani, kama utafanya *hili*, kama utafanya *lile*. . . " Limekwisha tayari, siyo, "Kama utaondoka ukapate elimu nzuri, kama utajua yote *haya*, *yale*, ama *mengineyo*. Mimi ni—nita—nitakuponya. Nitakuokoa kama ukipata Shahada ya Sanaa."

76 "Nimelifanya tayari; limekwisha. Ninakutaka tu unyoshe mkono hapa na ulipate. Hivyo tu." Mnaona ninalomaanisha? Ibra-. . . Jambo pekee lililompasa Ibrahimu kufanya lilikuwa ni kudumu katika agano Lake. Haikumbidi kufanya lolote kwa ajili ya hilo agano; Mungu alikuwa tayari amefanya hilo pamoja naye. Ilimbidi tu kubakia hapo. Haleluya! Sasa ninaanza kujisikia kubarikiwa. Mnaona?

77 Tunapojua jambo hili, kwamba jambo pekee tunalopaswa kufanya, kurithi yoyote ya ahadi za Mungu, ni kubakia papo kwenye Neno la Mungu, usiache chochote kikutikise kutoka Kwake.

78 Sasa angalieni, Yeye alikuwa mfano kamili wa Ibrahimu na uzao wake baada yake. Nami nitazifuatilia njia panda za maisha ya Ibrahimu, kisha nizifuatilie njia panda za uzao wa Ibrahimu, tuone kama Mungu alilitimiza Neno Lake herufi kwa herufi.

79 Sasa, Ibrahimu. . . Tunajua ya kwamba kuna njia moja tu ambayo tunaweza kuokolewa, na hiyo ni kuwa katika agano pamoja na Ibrahimu, kwa maana lilifanyiwa Ibrahimu. Lakini Biblia ilisema, "Sisi tukiwa ndani ya Kristo, sisi tukiwa wafu katika Kristo tunauchukua uzao wa Ibrahimu nasi ni warithi pamoja na Ibrahimu." Hiyo ni kweli? Sasa, Kristo ndiye Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Kutoka kwa Ibrahimu alikuja Isaka; kutoka kwa Isaka akaja Yakobo; kutoka kwa Yakobo akaja Yusufu; kutoka kwa Yusufu, kadhalika kuteremka, Daudi; Daudi na kuendelea; kuendelea; *fulani-na-fulani*; mpaka hatimaye ule Uzao wa Kifalme ukazaliwa ambao ulikuwa ni Kristo; na katika Kristo, ikamfanya Ibrahimu baba wa mataifa yote. Nalo agano la

Ibrahimu linathibitishiwa watu pasi-. . ., ama, linatolewa kwa watu pasipo na masharti.

80 Sasa, ukisoma sasa katika mlango wa 12, Yeye alifanya agano na Ibrahimu pasipo na masharti. Yeye alimwita Ibrahimu. Niliwasikia watu wakisema, "Mimi nilimtafuta Mungu, na nikamtafuta Mungu, na nikamtafuta Mungu." Umekosea. Mungu alikutafuta, na kukutafuta, na kukutafuta. Haikuwa ni wewe ukimtafuta Mungu; ni Mungu akikutafuta.

Mbona, mwanzo wenyewe ulilithibitisha. Adamu, ilipaswa kuwa ni Adamu akipaza sauti, "Baba, Baba uko wapi? Nimetenda dhambi, nimetenda dhambi, Baba."

Lakini ilikuwa ni Mungu akisema, "Adamu, Adamu, uko wapi?" Mnaona? Kwa hiyo daima ni . . .

Ungeweza kutoka nje na kumwambia nguruwe ya kwamba amekosea kwa kuwa anakula takataka? Angeamini hilo? La, bwana. Yeye angekwambia, "Ashike lake."

81 Na hivyo ndivyo ilivyo na mwenye dhambi. Huwezi kumwambia lolote. Hatakusikiliza. Hata hataketi kanisani dakika tano kukusikiliza. Kwanza kabisa yeye ni nguruwe. Yeye ni mla mizoga, koho; hiyo ndiyo asili yake. Mnaona? Kwa hiyo hu—hu—huwezi kumwambia lolote, kwa kuwa hivyo ndivyo tu alivyo. Yeye ni koho. Hawezi kula vitu vizuri.

82 Sasa, angalieni. Ndipo unapopata hilo, yale Mungu aliyomwambia Ibrahimu . . . Yeye alimwita Ibrahimu, na kama uliwahi kuitwa, haikuwa ni wewe ukitafuta; ilikuwa ni Mungu aliyekutafuta. Na kwa neema ya Mungu Yeye alikuokoa, sio kwa sababu ulifanya jambo fulani, sio kwa sababu unastahili hilo, bali kwa sababu neema ya Mungu kwako ilifanya hivyo. Kila mtu anayeelewa hilo, aseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, tunaanza.

83 Sasa, ilikuwa ni kitu gani? Wakati Mungu alipomchukua mwanadamu na kumwita kwanza, hiyo ilikuwa ni nini? Kuhesabiwa haki. Ibrahimu kwa kuisikia Sauti ya Mungu ikisema naye, alimwamini Bwana Mungu. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, yeye alihesabiwa haki kwa imani, kwa kumwamini Bwana Mungu. Hivyo ndivyo tulivyo, uzao wa Ibrahimu? Warumi 5:1.

> *Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.* (Warumi 5:1)

Sasa, Ibrahimu alimwamini Mungu. Na ikahesabiwa kwake kuwa ana haki, ama, ikawekwa kwenye akiba yake kama haki.

84 Unafanyaje? Unasema, "Vema, mimi—mimi—mimi ni baadhi ya ninii . . . mimi—mimi ni akina Jones; ni—ni—ninaishi katika ninii fulani . . . " Hilo halina uhusiano wowote nalo. Mungu alikuita, nawe unaukubali huo wito. Na kwa imani yako, kwa kumkubali Kristo, ule Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu

unakuita wewe, ndipo unahesabiwa haki kwa imani. Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo njia pekee niijuayo. Hayo ni Maandiko kadri nijuavyo mimi. Ninajua nilikuwa mwenye dhambi, aliyevunda. Mungu alinikomesha katikati ya dhambi yangu na kubisha mlangoni mwa moyo wangu, [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani—Mh.] nami nikageuka nikaangalia nyuma, kasema, "Ni nani?"

Akasema, "Mimi ni Bwana wako."

Nikasema, "Basi Bwana nijalie nije."

Kamwe sikusimama na kusema, "Hei, Bwana, hei, uko wapi? Ninataka kuzungumza na Wewe kidogo." Mnaona? La, hufanyi hivyo. Mungu ndiye anayekusimamisha.

85 Kwa hiyo sasa, Mungu alikuita kwa neema, si yale uliyofanya, yale uliyoweza kufanya, yale utakayofanya. Endapo wewe ni uzao wa Ibrahimu, Mungu alinena nawe kwa neema Yake ya ajabu, kama tu alivyomfanyia Ibrahimu katika mlango wa 12 wa Mwanzo.

86 Sasa, sasa, kisha angalia: Mara Ibrahimu alipomwamini Mungu kwa kuhesabiwa haki (Kumwamini Bwana, tunahesabiwa haki.), mara Mungu akamwita Ibrahimu apate kujitenga kikamilifu na kutokuamini kwote. Hivyo ndivyo alivyofanya ndani yako? Jitenge na jamaa yako, na washirika wako wote; toka kwenye nyumba za karata; toka kwenye kumbi za dansi; achana na mambo ya ulimwengu. Mungu hudai utengano mkamilifu, kwa uzao wa Ibrahimu, maana hivyo ndivyo alivyomwita Ibrahimu.

87 Unakulinganisha? Chombo *hiki* ni Ibrahimu, chombo *hiki* kinawakilisha uzao wake baada yake. Nalo agano lilifanywa kwa wote wawili Ibrahimu na uzao wake baada yake. Basi kama vile Ibrahimu alivyoitwa kwa neema, kwa uteuzi, vivyo hivyo uzao wake uliitwa kwa neema na uteuzi. Mnaona? Waliisikia Sauti ya Mungu na kumwamini Mungu, ndipo ikahesabiwa kwake kuwa ana haki. Aliisikia Sauti ya Mungu katika baa, popote pale, ndipo akamwamini Mungu, naye Ibrahimu aliamriwa kuacha na kujitenga na mambo ya ulimwengu, vivyo hivyo na uzao wa Ibrahimu: wajitenge na uzao . . . ya mambo ya ulimwengu.

Kuhesabiwa haki kwa imani, tungeweza kudumu kwenye hilo alasiri nzima, bali inatupasa kuharakisha.

88 Sasa, kama tunavyoona, Ibrahimu kamwe hakutii kikamilifu. Sasa, ndivyo ilivyo kwa wengi wetu sisi watu. Mara tunapoenda na kufanya ungamo, tunafikiri, "Vema, sasa, tumejiunga na kanisa nasi tutakuwa watu wazuri sana. Sisi ni majirani. Haitadhuru kuvuta sigara kidogo." Ama, "Loo, kama nikiendelea tu na karamu yangu ya karata, niende, hilo halitadhuru kitu." Bali kumbuka, Mungu kamwe hakumbariki Ibrahimu mpaka alipotii kikamilifu. Wala Mungu hataubariki

uzao wake mpaka utakapotii kikamilifu, kujitenga na mambo ya ulimwengu.

89 "Tokeni miongoni mwao. Mkatengwe nao," asema Bwana. "Nitawapokea. Msiguse vitu vyao vichafu. Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Mnaona?

90 Sasa mnaona, hamna budi kutoka ulimwenguni. Lakini Ibrahimu alifanya nini? Loo, aliambatana na mpwa wake, Lutu, mfuasi wa kanisa, vuguvugu; na babaye, mzee huyo alikuwa ni kikwazo, almuradi alikaa karibu naye; na—naye akachukua baadhi ya vitu akaenda navyo. Na hivyo ndivyo tu tunavyojaribu kufanya. Tunajaribu kuvuta tukaingiza makanisani, dhehebuni mwetu, mambo ya ulimwengu.

91 Sasa, ndugu zangu Wamethodisti, ninawapenda. Ndugu zangu Wabaptisti, ninawapenda, kama tu ninavyowapenda ndugu zangu Wapentekoste, ama wowote wale. Lakini mnaona, tunajaribu kuvuta mambo ya ulimwenguni, na kwenda nayo moja kwa moja kama Ibrahimu alivyofanya. Siwaondolei ukristo kwa dhehebu lenu. Ninawaambia tu, humtii Mungu kikamilifu mpaka utakapojitenga.

92 Sasa, wakati mngali mnakimbia kwenye maonyesho ya sinema kuona kila namna ya sinema ya kale, mnapokaa nyumbani na kuiachilia mikutano yenu mapema usiku wapate kuona kipindi fulani kisichokaguliwa cha televisheni, ili mweze kushuka kwenye chumba chenu cha chini, na baadhi yenu makanisa ya Kiprotestanti mnafanya hivyo, na kucheza michezo ya Karata na kadhalika kwenye chumba cha chini, milo ya supu usiku, maskini madansi ya kirafiki, kwenye kile kinachoitwa "YMCA," mkifundisha roki.

93 Basi sikilizeni. Ninyi, ndugu zangu wa Kimethodisti, wakati yapata majuma sita yaliyopita, mama yangu (Yeye ni Mmethodisti pia.), wakati aliponiita huko chini nyumbani, na hapa Indiana wao wakiwa na dansi ya roki katika kanisa la Methodisti kwenye televisheni, wakifunika taratibu za mambo kama hayo, nao walimwuliza nanii . . . hata mdhamini wa m—mtu huyo wa televisheni alisema, "Hivi huoni hili linapaswa . . . wa—watu wangekukosoa?"

94 Kasema, "Muda mrefu kupita kiasi kanisa la Methodisti lilisahau sanaa ya kupendeza ya roki." Kama John Wesley angalijua hilo, angalipinduka kaburini mwake. Mmeyaendea mambo ya ulimwengu kupita kiasi. Mnajua nini? Ninyi Methodisti . . .

95 Nilizungumza na Jack Shuler. Huyo ni mmoja wa—mmoja wa watu walio bora sana mlio nao. Mna mamilioni ya watu wazuri, watu wa kanisa la Methodisti, baadhi ya walio bora sana. Ninaangalia usoni mwa wahudumu wawili Wamethodisti, sasa hivi, ambao ni marafiki wasiri wangu. Hakuna watu bora zaidi

wanaosimama katika viatu vya ngozi, nijuavyo mimi. Hiyo ni kweli. Bali mnasahau; hamjitengi.

96 John Wesley ndiye aliyeanza kuhubiri utakaso, na kujitenga mwenyewe na mambo ya ulimwengu. Nanyi wanawake Wamethodisti mnaovaa kaptura, vipodozi usoni mwenu, kwani hamjui yale mwanzilishi wenu aliyosema kuhusu upuuzi kama huo? Lakini mna mimbara dhaifu na jengo kubwa. Hiyo ndiyo shida yenu. Wala msiangalie tu huku na kuwacheka Wabaptisti, maana, Wabaptisti, ninyi ni vile vile. Na, Wapentekoste, ninyi ni vile vile. Sasa, hatuna budi kulifanya sawa, sasa ni hayo tu.

97 Sasa, ni jambo la kusikitisha jinsi gani. Hivi hamjui ya kwamba kama ninyi ni uzao wa Ibrahimu, inawapasa kujitenga na mambo ya ulimwengu, maana lilifanywa kwa ajili ya Ibrahimu na uzao wake baada yake? Wala Ibrahimu kamwe hakuingia kwenye baraka. Si ajabu, kwenye maeneo haya hapa, huko kwenye Chuo cha Wheaton, huko chini Asbury, huko kwa Moody ambako tunaelekea tena, huko Chicago kwa Moody, ni kwa nini hawana miamsho kama walivyozoea kuwa nayo? Hamjitengi, enyi wana wa Ibrahimu. Mungu kamwe atafanyaje kazi mahali kama hapo, wakati Yeye hata hawezi kuwafanya muishi kimaadili? Hiyo ni kweli. Yeye kamwe hawezi kuwa na uamsho uliowekwa msingi juu ya upuuzi kama huo.

Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, unatukasirikia." Bwana na awe Hakimu wangu. Mnaona?

98 Lakini endapo mtu fulani hatawaambia, endapo jambo fulani halitukii, mtaishia huko ng'ambo mwishoni mwa maskini huo udanganyifu. Sasa, ondokeni kwenye kitu kama hicho. Ninyi, ninyi ambao. . . Vipi kuhusu kanisa la Methodisti, ninyi Wamethodisti, walipokuwa wakishuka kwenda barabarani, nanyi Wamethodisti hapa, mlipokuja kwa mara ya kwanza, wakati Asbury alipokuwa hapa, nanyi mlikuwa na mikutano ya mtindo wa kale wakati watu walipoanguka sakafuni kwa Roho Mtakatifu, wakiombea kule, wakirusha mateke na kupiga makelele na kutupa mikono yao juu, nanyi mngewamwagilia maji nyusoni mwao na vitu kama hivyo mpate kuwarejesha? Loo Mungu! Wamethodisti, ilikuwaje kwa tukio hilo? Liko wapi siku hizi? Ni jambo gani lililotukia? Jambo fulani lilienda kombo. Mnaona, mnachukuliwa na mkondo kwenye. . . Mnaondoka kwenye njia mbali na uzao wa Ibrahimu.

99 Sasa angalieni, Mungu, jambo lingine. . . Sasa huko kulikuwa ni kuhesabiwa haki. Kuharakisha. Sasa, Mungu alifanya nini sasa katika Mwanzo 12? Alimwokoa Ibrahimu kwa uteuzi, naye Ibrahimu akahesabiwa haki kwa imani, akiliamini Neno la Mungu. Hiyo ni kweli? Wabaptisti, hivyo ndivyo mlivyolipata? Wamethodisti, hivyo ndivyo mlivyolipata? Wapilgrim Holiness, Wanazarayo, Wapentekoste, hivyo ndivyo

mlivyolipata? Hakika, kweli kabisa. Sasa, angalieni kiwango cha ile safari; wakazidi kwenda.

100 Kuharakisha sasa, ninataka mwandamane nami kwenye mahali hapo pengine sasa katika Mwanzo 15. Mambo mengi sana mle ndani tungeweza kuchukua juma, juma, na juma baada ya juma juu yake, lakini kuzileta tu hatua hizi kwenu kuwaonyesha yale Yeye aliyofanya.

101 Katika mlango wa 15 Ibrahimu alianza kushangaa, "Nitapataje kujua mambo haya." Ndipo Mungu akamthibitishia lile agano. Akampa thibitisho la lile agano. Katika Mwanzo mlango wa 15 tunaona hilo; hapo alipojitenga kikamilifu, Lutu alishuka akaenda Sodoma, naye yule mzee akafa, naye Ibrahimu akajitenga na kukaa peke yake, ndipo Mungu akaanza kusema naye.

102 Wabaptisti, fanyeni hivyo! Wamethodisti, fanyeni hivyo! Wapentekoste, fanyeni hivyo! Jitengeni na mambo ya ulimwangu muone kama Mungu hataanza kusema nanyi. Jitengeni na mambo ya maisha haya muone kama Mungu hatasema nanyi. Lakini wakati alipofanya hivyo kikamilifu, yeye alisema, "Sasa, angalia kwamba Wewe ulinipa ahadi ya mwana, nami sina mtoto, na mrithi wangu wa pekee ni huyu Eliezeri wa—wa Dameski," kasema, "nitakuwaje . . . itakuwaje?"

103 Sasa, sikilizeni kwa makini ninyi nyote. Sasa, hapo, Ibrahimu, katika Mwanzo 1, alihesabiwa haki kwa imani. Sasa, hili hapa fundisho lenu la John Wesley linakuja. Huu hapa utakaso we—wenu unaingia, ama kuthibitishwa kwenu kwa lile agano.

104 Kumbukeni, Ibrahimu alichukua mbuzi jike, ndama, na . . . wanyama watatu: mbuzi, kondoo, ndama, wa miaka mitatu, hao watatu wakiwa ni thibitisho, zile tatu-tatu nilizowaambia tena mshikilie, umri wa miaka mitatu. Basi akawachinja na kuwapasua vipande-vipande. Hiyo ni kweli?

105 Kisha akachukua hua na njiwa ambao wanawakilisha uponyaji wa Kiungu, kamwe hakuwapasua. Mnaona hilo? Kamwe hakuninii . . . Biblia ilisema yeye . . . Wakati unaposoma hili huko nyuma sasa nikiisha kuondoka, yeye kamwe hakupasua njiwa na hua, kwa sababu gani? Kulikuwako na badiliko katika agano kutoka kwa Kristo kwenda kwa ninii . . . kutoka kwa mwana-kondoo kufikia kwa Mwana-kondoo wa Mungu, lakini uponyaji wa Kiungu daima umewekwa msingi juu ya imani yako. Kamwe hakuwapasua hua na ndege. Yeye aliwaweka pale chini, bali kweli alizipasua zile dhabihu za miaka mitatu.

Sasa, ilikuwa ni kitu gani? Kule kumwagwa kwa damu.

106 Wa kwanza wa uzao wa Ibrahimu katika wakati wa kanisa . . . Mnaamini wakati wa kanisa ulianza baada ya Pentekoste? Mnaamini ile zamu ya kwanza pale, ya Wayahudi,

na kadhalika? Basi mnaamini matengenezo ya kwanza ya kanisa lililoitwa litoke kwa ajili ya Unyakuo lilikuwa ni kundi la Kilutheri? Hakika ndivyo. Yeye alihubiri, "Wenye haki wataishi kwa imani." Yeye alikataa kwamba ushirika ni mwili halisi wa Kristo na kuutupa sakafuni, yule kasisi kijana Martin Luther, na kuhubiri, "Wenye haki wataishi kwa imani." Hiyo ni kweli?

John Wesley alihubiri utakaso, kazi ya pili dhahiri ya neema (Hiyo ni kweli?), akijitenga mwenyewe na mambo ya ulimwengu.

107 Sasa, Yeye alimshughulikia Ibrahimu chini ya kuhesabiwa haki. Kisha uzao wa Ibrahimu ulikuwa ni Martin Luther chini ya kuhesabiwa haki. Sasa, Yeye anamjia Ibrahimu kwa thibitisho la lile agano na pia anakuja huku kwa uzao wa Ibrahimu katika thibitisho la agano kwa ajili ya kurudi kwenye ile Damu, kule kuchinjwa kwa ile Dhabihu. Loo, mnaliona? Semeni, "Amina" kama mnaliona.

Sikilizeni, ndipo Yeye anarudi kwenye ile dhabihu. Angalieni, hebu nichukue dakika moja tu jinsi ambavyo hiyo dhabibu ilithibitishwa. Kisha tutaharakisha.

108 Sasa, angalieni upesi. Tunafanya namna gani tunapothibitisha a—agano? Ninasema kwa, ndugu *huyu hapa*, hebu simama kwa dakika moja. Wewe ni mchungaji, unalo kanisa? Unasema, unalo kanisa? [Ndugu huyo anasema, "La, mimi ni mwinjilisti."—Mh.] Vema.

109 Aisee, *wewe* unalo kanisa? Vema, hebu simama kwa dakika moja tu. Una—unalo kanisa. Unasema, "Ndugu Branham, hebu twende tukale chakula cha mchana pamoja."

"Vema."

"Utakuja kanisani mwangu na kufanya uamsho?"

"Umm. Hebu tuone. Loo, na—nakwambia tutakalofanya. Tutafanya jambo *fulani-fulani*."

"Naam, nitafanya hivyo."

110 "Nipe mkono, jamani; jambo ndilo hilo. Nitakuwa papo hapo." Ndivyo ilivyo? Hivyo ndivyo tunavyothibitisha maagano yetu (Hiyo ni kweli?) kwa kupeana mkono: tunakula kitu kidogo, tunapeana mkono. Tutakubaliana. Hiyo ndiyo ahadi yetu mmoja kwa mwingine, mkono wetu wa kuume, "Uweke hapa; tutalifanya." Hilo ni agano Marekani.

111 Vema, mnajua jinsi wanavyolifanya huko Japani? Wanatoka wanaenda kula chakula kidogo, ndipo wanaporudi, nao watafanya, watalithibitisha agano lao, wanachukua chombo kidogo cha chumvi, nao wanasimama na kurushiana chumvi mmoja kwa mwingine. Hivyo ni, chumvi ni mawasiliano, ladha (Mnaona?), ambalo linamaanisha ya kwamba wao. . .hivyo ndivyo wanavyothibitisha agano lao.

112 Lakini mlijua jinsi walivyolifanya huko mashariki katika siku za Ibrahimu? Ninatumaini ya kwamba sirarui chochote cha thamani; maskini barua hii hapa iliyo na leso ndani yake, lakini ninataka kutumia kitu fulani. Walizichukua dhabihu hizo na kuchinja dhabihu. . . Ninatumaini mnaelewa, ninazo hapa zile dhabihu tatu, ilikuwa ni wakati huu, ikimaanisha zile jamii tatu, vizazi vitatu, *fulani na fulani* na kuendelea. Sasa, sisi . . . Nyakati tatu za kanisa na kadhalika za mwisho wa kuitwa kwa Kanisa.

113 Ndipo wanaichinja dhabihu hii; wanakusanyika, na juu ya karatasi ya ngozi ambayo ilikuwa ni ngozi ya kondoo, wakaandika: "Nitakubali kufanya *hivi na hivi na hivi* pamoja nawe."

"Naam, tutafanya hilo." Vema. "Utatimiza jukumu hili?"

"Naam. Nitalitimiza." Vema. "Utafanya *hivi na hivi*?"

"Naam, nitafanya, nitalitimiza."

114 Vema, wanaichinja dhabihu; wanasimama moja kwa moja katikati ya dhabihu hizi, wanamwinulia Mungu mikono yao, na kutoa nadhiri: Kama wakilivunja agano hili, mwili wao na uwe kama mzoga huu ulio hapa. Halafu wanaichukua hii na kuirarua. Mmoja anachukua kipande kimoja na mwingine anachukua kipande kingine. Sasa, hakuna njia ulimwenguni ya kukishikamanisha hicho tena. Hakina budi kuwa ni kitu kile kile wakati tutakapokutana pamoja. Nina kipande changu cha hicho; yeye ana kipande chake.

115 Sasa, Mungu alifanyaje? Alikuwa akitaka kumwambia yale Yeye atakayofanya, jinsi atakavyolifanya kupitia kwa Dhabihu, jinsi atakavyomfanya yeye baba wa mataifa, na hata hivyo hakuwa amempa jina hilo bado, bali alikuwa anataka kumfanya baba wa mataifa, naye akaichinja ile dhabihu, akimzungumzia katika hili.

116 Sasa angalia. Ibrahimu aliona nini? Jambo la kwanza baada ya kuichinja ile dhabihu, yeye aliwafukuza ndege wasiikaribie mpaka jua lilipokuchwa. Jua lilipokuchwa, kulifanyika nini? Usingizi mzito ulimshika Ibrahimu. Hiyo ni kweli? Mwanzo 15. Usingizi mzito juu ya Ibrahimu. Hiyo ni nini? Mauti kwa kila mwanadamu, uzao wote wa Ibrahimu.

117 Ni jambo gani lililotukia baada ya huo usingizi mzito? Ndipo hofu nyeusi ikaja mbele zake. Ndipo kutoka kwake ikaja tanuru ya moshi, ambapo kila mwenye dhambi huenda kuzimuni. Lakini baada ya hiyo ikatokea Nuru ndogo nyeupe na maskini Nuru hii ikapitia katikati ya ile dhabihu. Kasema, "Unaona nitakalomfanyia, Ibrahimu?" Nuru ndogo, Mungu ni Nuru. Naye akapitia katikati ya dhabihu hii, vipande hivi vya mzoga hapa. Alikuwa akifanya nini? Akifanya agano. Aliapa kwa nani? Nafsi Yake. Asingeweza kuapa kwa yeyote aliye mkuu zaidi. Sikuzote unaapa kwa mtu aliye mkuu kuliko wewe. Kwa hiyo hakuna mtu, Biblia ilisema, ambaye Yeye angeweza kuapia, maana Yeye ndiye

aliye mkuu kuliko wote, basi akaapa kwa nafsi Yake (ati nini?): Yeye atatimiza lile agano pamoja na Ibrahimu na uzao wake. Haleluya!

118 "Nitaapa kwa nafsi Yangu ya kwamba sitakiuka Neno moja kutoka kwenye agano Langu pamoja nawe ama uzao wako baada yako." Vipi kuhusu hilo, dada? Vipi kuhusu hilo? "Nitatimiza Neno Langu." Akaapa kwa nafsi Yake, Biblia ilisema aliapa. "Nitalitimiza agano Langu. Nitakuapia, Ibrahimu, nitafanya hilo."

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ndugu washika sheria, simaanishi kufinya sana, ila ninataka tu kusema jambo moja hapa, kwa dakika moja tu.

119 Angalieni hapa, angalieni yale Yeye aliyofanya. Alifanyaje jambo hilo? Alikuwa akizungumzia kitu gani? Hakika ninyi ni wa kiroho vya kutosha kulishika. Yeye alifanya nini? Kristo alikuwa ndiye ule Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu ulioahidiwa. Hiyo ni kweli? Yeye alifanyaje na Yeye? Alimpeleka Kalvari.

120 Yeye aliishi duniani. Alithibitisha alikuwa ni Masihi kwa ishara na maajabu, kuzijua siri za moyo, kutambua mawazo yao, akithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi ajaye. Tumelifundisha hilo juma hili? Biblia imesema hivyo? Neno la Mungu lilisema hivyo? Yeye alithibitisha alikuwa ni Masihi.

121 Yeye alifanyaje na Yeye? Alimpeleka Kalvari na kumpasua, akaufufua mwili Wake kwenye siku ya tatu kwa ajili ya sehemu Yake, na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume, ndipo akamtuma Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Kristo akalishukia Kanisa Lake (Haleluya!) lipate kufanya kazi ile ile na jambo lile lile alilofanya Yeye.

122 Agano lako liko wapi, kipande chako cha umiliki? Wakati hilo Kanisa halisi sana la Yesu Kristo litakapokuja kukutana kwenye ule ufufuo, Roho yuyo huyo aliye ndani ya Kristo itambidi kushikamana na agano lile lile. Sijali ni hadithi ya aina gani uliyo nayo pamoja na Methodisti, Baptisti, Pentekoste, chochote ulicho nacho, iwapo Roho wa Kristo hayuko ndani yako, basi wewe si uzao wa Ibrahimu, wala huko kwenye lile agano. maana hapo ndipo Yeye alipoliandika lile agano. Amina.

123 Kama hukubaliani nalo, soma Biblia yako. Basi Roho, Roho aliye juu ya Kristo yuko juu ya Kanisa. "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi. . ." *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. ". . .Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Nazo kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Nitakuwako mpaka mwisho wa ulimwengu. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

124 Aibu kwenu ninyi Wamethodisti msioamini, ninyi Wabaptisti msioamini, ninyi Wapentekoste msioamini, mnaodai kuwa uzao wa Ibrahimu kisha mnabishana na Neno Lake, ati "Siku za miujiza zimepita." Mungu aliapa kwa kiapo Yeye

angeudumisha uzao huo hai kupitia kwa kila taifa kupitia kwa kila kizazi: Uzao wa Ibrahimu. Amina. Lakini kwa ile damu, Yeye alilithibitisha katika mlango wa 15.

125 Sasa, hebu twendeni mbele zaidi kidogo. Yeye alifanya nini? Kuhesabiwa haki basi kwa imani, kwa kuamini: Kuhesabiwa haki kwa uzao Wake (Hiyo ni kweli?) kupitia kwa Martin Luther. Kutakaswa kwa damu, hiyo ni kweli? Kutakaswa kwa Kanisa Lake kwa John Wesley. Sasa nini? Ibrahimu yuna umri wa miaka mia moja.

126 Fungua ukurasa ufuatao katika Biblia yako, mlango wa 17. Angalia kama Mungu hulitimiza Neno Lake. Ibrahimu ni mzee. Ana umri wa miaka mia moja, alikuwa hivyo, kasoro mwaka mmoja; alikuwa tisini na tisa. Ndipo Bwana akamtokea katika Jina la *El-Shadai*, "kifua."

127 Kunradhi, enyi wasichana, dada zangu. *El*, linatokana na neno "Mwenye nguvu"; *Shad* linamaanisha "titi." *Shadai* linamaanisha "mwenye matiti." Mungu, Yeye alisema, "Mimi ni Mwenyezi Mungu."

128 Sasa, kama una *Biblia ya Scofield*, ama kama una *Thompson Chain*, ama kama una *Emphatic Diaglott*, ama chochote cha maoni, utaona ya kwamba neno hilo lilitenganishwa wakati alipomwita hivyo, yeye alimwita "El," na Yeye akamtokea katika Jina la El-Shadai. Ni ujumbe mzuri jinsi gani kwa mzee ambaye alikuwa akiiamini ahadi ile, sasa, kwa muda wa miaka ishirini na minne. Ndipo Biblia ikasema, "Yeye alipata nguvu wakati wote."

"Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, tutampata."

Miaka kumi na mitano ikapita. "Utajisikiaje, Sara?"

"Vema, kamwe si—si—sina tofauti yoyote. Mimi. . . "

129 Sikilizeni nitakuwa dhahiri kabisa, nanyi msikilize. Mnaona, yeye alikuwa amekoma kuwa mama, ama, kuwa mwanamke, mwajua, zile siku ishirini na nane, tangu wakati alipokuwa msichana mdogo, zinakoma kwenye yapata umri wa miaka arobaini, arobaini na mitano; ndipo Mungu alipomwita, yeye alikuwa ameupita huo kwa miaka thelathini, ishirini. Sasa angalieni mahali alipo. Ana umri wa miaka sabini na mitano. Naam, ana zaidi ya hiyo; ana umri wa miaka themanini na mmoja. Lakini angalieni, badala ya Ibrahimu kuwa dhaifu. . . Mko tayari? Badala ya Ibrahimu kuwa dhaifu hapo alipoona halikutukia, Biblia ilisema alitiwa nguvu. Amina.

130 Na hapa halina budi kutukia katika dakika moja la sivyo tunasema, "Mnaona, niliwaambia, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Nilipoteza uponyaji wangu." Wewe ni mfano duni wa uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu huamini tu

kama Ibrahimu alivyoamini. Haidhuru nini, ni muda gani, kile chochote kisemacho, ndivyo ilivyo kwa vyovyote vile. Mungu alisema hivyo. Ibrahimu na uzao wake baada yake . . .

131 "Vema, nitakwambia, Ndugu Branham, sistahili uponyaji." Ndio kwanza tu nimalizie kuwaambia, si lolote ulilofanya, ni yale Yeye aliyofanya. Wewe endelea kuwazia hustahili.

132 Hapa, vipi kama maskini farasi jike nyuma katika wakati wa Biblia, angalimzaa ma—maskini mwanafarasi dume? Ama alikuwa na . . . Tuseme alikuwa na nyumbu. Naye nyumbu huyu alizaliwa, na masikio yote mawili yaliinama chini; mkia wake umechomoza juu kabisa; macho yake yana makengeza; magoti yake yana matege. Vema, kama angaliangalia kwenye kioo na kuwazia, angesema tu, "Ole wangu. Kamwe hawatanilisha. Watanipiga tu kichwani watakapotoka nje na kuniona."

133 Lakini vipi kama mama yake alikuwa amefunzwa vizuri katika sheria? Angesema, "Ngoja kidogo, kipenzi. Ngoja kidogo. Ninajua ya kwamba wewe ni kiumbe kinachoonekana cha kuchukiza sana. Hufai kitu, bali utaishi. Kwa sababu kuna sheria ya Mungu inayosema umezaliwa chini ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Wewe ndiye kifungua mimba wangu." Ee Mungu!

134 Kwa nini unataka kuwa Mpresbiteri? Kwa nini usirudi na kuwa Mpentekoste kama ilivyokuwa hapo mwanzo, ile haki ya mzaliwa wa kwanza? Unaweza kuwa Mpresbiteri wa Kipentekoste. Unaweza kuwa Mmethodisti wa Kipentekoste. Rudini kwenye kanisa la kwanza, jinsi lilivyoanza.

135 Mseme, "Ulizaliwa chini ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Nitakwambia: Kama ulizaliwa chini ya haki ya mzaliwa wa kwanza, unajua kitakachotukia, kitakachotendeka? Asubuhi wajapo malishoni kukuona? Unajua watakalofanya? Hawatakugonga kichwani, kwa sababu utaishi, lakini wataninii . . . wataunyosha mkono na kumshika mwana-kondoo asiye na hatia." Amina. "Nao watamchukua mwana-kondoo huyo asiye hata na lawama juu yake, naye mwana-kondoo huyo itambidi afe badala yako. Kuhani kamwe hatakuona." Amina.

136 Mnaliona? Usijiangalie mwenyewe; iangalie Dhabihu yako. Mungu hakuangalii; Yeye anaiangalia Dhabihu yako ambayo ni Kristo. Usijiangalie mwenyewe. Mimi sistahili; wewe hustahili; hakuna mtu anayestahili; bali Yeye Ndiye. Sihesabu yale nimefanya, kile nilicho mimi, la sivyo ni—nisingefaulu. Lakini ninaangalia yale Yeye amefanya. Hapo ndipo ninapotumainia: Yale Yeye amefanya. Yeye ndiye Dhabihu yangu. Sistahili uponyaji. La, bwana. Bwana, nilipaswa kufa muda mrefu uliopita, kamwe sikustahili hata kuzaliwa. Ila ninaishi; ninao Uzima wa Milele; ninaenda Mbinguni. Kwa nini? Kwa maana Yeye alilifanya kwa ajili yangu. Alikuwa Ndiye. Alichukua mahali pangu. Nilikuwa na matege, mwenye makengeza katika hali ya kila namna, bali Yeye alipachukua mahali

pangu. Tukinena kiroho, nilikuwa nimepindika kabisa, na kuvurugika kabisa; bali Yeye akapachukua mahali pangu; kwa hiyo Yeye ananifanya mwana mkamilifu wa Mungu, binti mkamilifu wa Mungu. Dhabihu Yake ilifanya hilo, si yangu. Sikuwa na uhusiano wowote nalo. Nilizaliwa nimeumbuka kabisa kwa vyovyote vile. Lakini si—situmaini katika yale nimefanya. Ninatumaini yale Yeye amefanya (Mnaona?), kile Yeye alichokuwa, hivyo ndivyo ilivyokuwa.

137 Sasa, Yeye alimwambia nini Ibrahimu? "Wewe ni mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, Ibrahimu. Wewe una tisini na tisa. Ila mimi ni El-Shadai; mimi ni Yule Mwenye matiti."

138 Sasa, tuko kwenye...Tulipita njia panda ya kwanza, kuhesabiwa haki: kuhesabiwa haki; kutakaswa: kutakaswa. Sasa kumbukeni, hayo yalikuwa ndiyo mambo ambayo Mungu aliahidi na kumfanyia Ibrahimu, bali hapa Yeye alisema, "Mimi ni Mungu mwenye matiti. Sasa, wewe ni mzee, Ibrahimu. Una umri wa miaka mia moja, bali kwangu Mimi wewe si zaidi ya mtoto mchanga. Kwa hiyo ninakupa ahadi, na mimi ni Mungu mwenye matiti. Mimi ni Mwenye nguvu. Egemea kifuani Mwangu sasa ukazinyonye nguvu Zangu ziingie katika mwili wako dhaifu," akimwandaa kwa ajili ya ule mwujiza.

139 Hivyo ndivyo alivyowafanyia Wapentekoste baada ya wakati wa Wesley. Aliwaacha Wapentekoste wazinyonye nguvu Zake Mwenyewe, Roho Wake Mwenyewe Mtakatifu kama ubatizo, kurudi kwenye miili yao dhaifu wapate imani kwa ajili ya Unyakuo, kuwapa imani kwa ajili ya miujiza. "Mimi ni El-Shadai."

140 Yale aliyomfanyia Ibrahimu na kwa uzao wake baada yake, angalieni: kuamini, kuthibitishwa, agano la damu, sasa akijiingiza Mwenyewe, nguvu Zake, ndani ya watu Wake.

Neno *kutakasa* lina maana gani, enyi Methodisti wema?

"Utakaso, unauamini, Ndugu Branham?"

Bila shaka ninauamini. Ni Neno la Mungu.

"Unamwamini John Wesley?"

141 Kabisa, yeye alikuwa ni malaika wa agano wa wakati wake, Wakati wa Filadelfia. Luther alikuwa mmoja wa Sardi huko nyuma. Hiyo ni kweli kabisa. Nasi tunaye mmoja ajaye ambaye atakuwa ni nabii. Yeye atakuwa ni Eliya. Kweli kabisa.

"Loo," mnasema, "yeye alinena juu ya Yohana pale."

142 La, la. Hiyo ni Malaki 3, "Nanii Wangu...Ninamtuma mjumbe Wangu mbele Zangu." Lakini kumbukeni, huyo—huyo Eliya alikuwa aje, ulimwengu ulikuwa uteketezwe kwa moto mkali kabla ya Kuja kwa Siku hiyo kuu ya Bwana; wala haukuteketezwa hapo awali, wakati Yohana alipokuja. Isome Biblia, ndugu. Unaona? Angalia yale atakayofanya, ninii... mwangalie jinsi, sehemu hiyo ya mwisho ya Malaki 4:

143 "Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao," Hiyo ni kweli? "na," kiunganishi, "mioyo ya watoto imwelekee baba." Mnaona huko kuja maradufu kwa Eliya?

144 Sasa, ninajua jamaa hawa husimama siku hizi na kusema, "Mimi ni Eliya; mimi ni Eliya; na mimi . . . " Loo, huo ni upuuzi. Angalieni. Angalieni yaliyotukia. Mioyo ya akina nani? Watoto, mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, kuja mara ya kwanza kwa Yohana, yeye aliigeuza mioyo ya baba wa kale wa kiorthodoksi ikaelekea kwenye huu ujumbe mchanga, wale watoto. Lakini katika kuja mara ya pili yeye ataichukua mioyo ya watoto sasa, na kuigeuza iirudie imani ya wale baba wa Kipentekoste hapo mwanzo, akijaribu kuirudisha.

145 Atakuwa mchukia wanawake, mpenda nyika. Hatakuwa mfuasi wa dhehebu lolote. Kasema, "Msifikiri kusema mioyoni mwenu, 'Tunaye Ibrahimu baba yetu.'" Wala Yohana, wala Eliya. "Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

146 Kamwe usiende na kuja na kusema, "Mimi ni Methodisti, Baptisti, ama Presbiteri, ama Pentekoste." Yeye ataliweka shina, mti . . . shoka kwenye shina la mti. Atajitokeza jukwaani moja ya siku hizi. Mwangalieni tu; wao watamchukia. Lakini baada ya Ujumbe wake, basi hukumu itaipiga nchi. Ataondoka aende mahali fulani kusudi hukumu iweze kupiga.

147 Kuna maskini mwanamke mdogo mle ndani, mnakumbuka. Naye alikuwa na mume, kiongozi mwanamume. Alikufa wakati Muungano wa Makanisa ulipolichukua. Wakati Eliya alipotoka, yeye alitumwa kwake, naye alifurahia kuupokea Ujumbe wa nabii wakati huo. Kwa hiyo akamlisha kwa msaada wa Mungu.

148 Sasa, mwangalieni Ibrahimu, akivuta, akijistawisha katika nguvu zote za Mungu (Ati nini?), akiingiza nguvu apate kujiandaa kumzaa mtoto huyu kwenye umri wa miaka mia moja.

149 Si kwamba tu Yeye ni Mwenye matiti, bali Yeye ni Mshibishaji. Mtoto mchanga wakati akiwa mgonjwa, na mgonjwa sana, mama humweka kwenye titi lake, naye anaanza kumnyonyesha huyo mtoto mgonjwa nguvu zake; na wakati akipata nafuu, anashiba. Vivyo hivyo na mtu halisi ambaye amemshika Mungu na anajilisha katika Roho Mtakatifu akijua ya kwamba ameridhika ya kwamba Mungu atafanya kila neno litimie. Yeye ni uzao wa Ibrahimu. Huyo ndiye uzao halisi wa Ibrahimu. Sijali mtu mwingine yeyote anasema nini; yeye anasema, "Kama Mungu alisema hivyo, hilo latosha; ninasema, 'Amina' kwake." Naye ameridhika litatukia. Wewe humrushi-rushi huku na huku.

Huenda daktari akasimama na kusema, "Hebu nichukue pigo lako la moyo. Unakufa."

"Sifi." Um-hum.

“Loo, umekumbwa kabisa na fadhaa. Vema, afadhali urudi ka—kazini mwako kwa maana hujaninii . . . Hakuna kitu kama huyo Roho Mtakatifu.”

150 “Hujui unachozungumzia. Nimemshika El-Shadai. Amina. Amina, ninajua ninaposimama.” Kila ibilisi angesimama na kutupa moto usoni mwake. Yeye bado asingelitilia shaka. Angeingia moja kwa moja kwenye tanuru inayowaka moto kama wale wana wa Kiebrania. Kwa nini? Yeye ni uzao wa Ibrahimu. Haidhuru inachukua muda gani, naye ameombewa, akapakwa mafuta, ama njia yoyote aliyopitia, yeye alikubali; kwa namna fulani imani inamwambia ya kwamba anaamini ataponywa. Ataponywa. Hakuna lingine. Anaamini ataenda katika Unyakuo; hakuna kitu kinachoweza kulikomesha. Anaamini Roho Mtakatifu yuko ndani yake, kwa sababu yeye anaona ishara halisi za Roho Mtakatifu.

151 Afadhali uache kuzungumza naye. Mfundishe tu . . . Unaweza kumfundisha thiolojia yote ulimwenguni; asingefanya hilo, kwa sababu . . . Asingelikuamini, maana anajua yale Biblia isemayo. Anajua ya kwamba ameshika Kitu kilicho halisi. Hapo ndipo Mungu alipompa . . .

152 Sasa, unaona yale aliyomfanyia Ibrahimu? Kuhesabiwa haki: Kuhesabiwa haki kwa Kanisa lake, uzao Wake. Kutakaswa kupitia kwa Wesley yule mjumbe mashuhuri: Utakaso, pia. Pentekoste kupitia *pale*: Pentekoste kupitia *hapa*. Mnaona? Pentekoste ikinyonya, ikileta . . .

153 Ni wangapi wanaofahamu ya kwamba wakati alipokuwa El-Shadai, ya kwamba Yeye alitoa nguvu Zake Mwenyewe akampa Ibrahimu. Kamwe hakufanya kitu ila kumpa ahadi, ahadi, bali hapa Yeye anajimwaga Mwenyewe ndani ya Ibrahimu, kikweli. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Vema, huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu. Kuhesabiwa haki ni yale unayoamini. Utakaso ni yale Damu iliyokufanyia. Unatakaswa kwa kuamini. Lakini unapojazwa kwa Roho Mtakatifu, ni Utu wa Roho Mtakatifu Mwenyewe, loo, ule Utu, sio mawazo, sio namna fulani ya saikolojia, bali Utu wa Roho Mtakatifu.

154 Na kwako wewe, ndugu yangu wa Sayansi ya Ukristo, nawe usiyeamini ya kwamba Roho Mtakatifu ni Mtu, *yeye* ni kiwakilishi nafsi.

Biblia ilisema, “Wakati Yeye, Roho Mtakatifu, ajapo, Yeye atashuhudia habari Zangu.” Yeye ni Mtu si wazo.

155 Alinyonya, si kutoka kwenye vile vitu na kutoka kwenye ahadi, lakini alikuwa, sasa, na Uzima halisi wa Mungu ukitiririka ndani yake. Hivyo ndivyo wakati wa Kipentekoste ulivyofanya. Sasa, yeye alifanyika nini basi? Mwana. Amina.

Sasa, katika Agano la Kale tunajua . . . Sasa, tuna yapata dakika kumi na tano tu zaidi.

Tunajua katika Agano la Kale, ni kitu gani kilichotukia? Katika Agano la Kale kulikuwako na kitu kama mwana kuzaliwa katika nyumba fulani.

156 Sasa, hakikisheni mnalipata hili. Mnasikia? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninajua mnafikiri nina kichaa alasiri ya leo ama labda wakati wote, bali ninawataka mlipate.

157 Sasa, angalieni yale aliyofanya. Mtu alipozaliwa, ama mtoto alipozaliwa katika familia, yeye alizaliwa akiwa ni mwana. Hiyo ni kweli? Bali hakuwa na urithi bado. Ilimbidi kufunzwa. Hiyo ni kweli? Sasa, unapompokea Roho Mtakatifu. . . Hapo ndipo Pentekoste ilipofanya kosa kubwa. Kasema, "Utukufu kwa Mungu, tunaye. Hakuna lingine." La, la. La, la, la, la, la, la, la, la, la.

158 Katika Biblia wakati mtoto mchanga alipozaliwa kwenye shamba la m—mtu, yeye alienda akamwajiri mwalimu aliye bora sana aliyeweza kumpata. Nitawaambia wonyesho wake wa kupendeza, ni mlango wa 17 wa Mathayo Mtakatifu, ule Mlima wa Kugeuka Sura, mkitaka kuuandika huo na kuusoma. Jinsi Mungu alivyomfanya Mwana Wake Mwenyewe kama tu vile hasa. . . Mungu haninii. . . Yeye hana budi kutimiza sheria Zake Mwenyewe. Hawezi kuharibu sheria Zake Mwenyewe ama kuzivunja sheria Zake Mwenyewe. Hawezi kuwa ni Mungu na mwenye haki na kufanya hivyo. Naye hana budi kuzitimiza apate kuwa mwenye haki, na mtakatifu, na wa haki. Angalieni vile Yeye alivyofanya sasa.

159 Mtoto mchanga hapo alipozaliwa, baba yake alikuwa na shughuli nyingi, kwa hiyo alimwajiri mwalimu aliye bora sana angaliweza kumwajiri kumlea huyo mtoto. Ndipo huyo mwalimu akamletea baba neno jinsi mtoto alivyokuwa akiendelea. Hiyo ni kweli, ndugu? Tunajua katika Wagalatia, pale, na mahali mbalimbali, ambapo Maandiko yananena habari zake. Nako kuliitwa "kumweka mwana." Sasa sikilizeni tu kwa dakika zingine chache.

160 Sasa, vipi kama huyo mwalimu alikuja. . . Sasa, kumbukeni baba alimpata nanii. . . Kama yeye alimpenda mvulana huyo, angempa mwalimu aliye bora kuliko wote aliyeweza kumpata. Unaamini hilo? Huyo alikuwa ni mwanawe. Sasa, hakutaka kununua. . . kumpata mwalimu pale ambaye angetaka kumpendeza bure na kumwambia uongo kuhusu huyo mtoto. Alitaka kujua yale hasa yaliyokuwa yakiendelea kwa mtoto huyo, kwa hiyo akamwajiri mwalimu mzuri kweli. Naye huyo mwalimu angekuja. Sasa kama ba-. . .

161 Kama mvulana huyo alikuwa akiendelea na kufanya vema, jinsi ambavyo hapana shaka huyo mwalimu alijisikia, akienda na kusema, "Aisee, sawa." Lakini vipi kama mwalimu huyo angeninii tu. . . vipi kama mvulana huyo alikuwa ni mwasi tu,

asingesikiliza, asingefanya chochote kuhusu baba, jinsi ambavyo mwalimu hapana shaka alijisikia wakati alipojongea na kusema, "Aha, naam, bwana, ah, uhu, yeye hafanyi vizuri sana. La, bwana, yeye ni . . . Sa—sa—samahani, bali hafanyi vizuri sana."

162 Sasa, ewe mfuasi vuguvugu wa kanisa, nitakumwagilia vizuri sana. Unafikiri nini wakati Mungu alipomweka mtoto Wake hapa, kanisa, ni Mwalimu wa aina gani Mungu alimpatia? Askofu? Huh? Papa? Yeye alimtuma nani akamlee mtoto Wake? Roho Mtakatifu. Askofu atazembea na kutaka kutiwa ua kwenye kofia yake apate kuwa askofu mkuu na—na kila namna ya waangalizi wa jimbo, na namna hizi zingine zote za mambo, bali Roho Mtakatifu ataleta ujumbe wa kweli mbele za Baba. Naam, bwana.

163 Kwa hiyo unafikiri Roho Mtakatifu atajisikiaje wakati anapokuja mbele za Baba na kusema, "Wanawake Wako wa Kipentekoste wanakata nywele zao, Baba. Wanajipodoa kama hao wengine wafanyavyo. Hawaendi kwenye mkutano wa maombi tena. Wanao hawatahubiri dhidi yake."

"Kuna shida gani? Kuna shida gani?"

164 "Loo, wameingia katika miradi mikubwa ya ujenzi. Nao hawatambui ya kwamba nilisema, ya kwamba, 'Naenda kuwaandalia Mahali.' Naam, wanakuwa wasioweza kuondoka duniani. Naam, wanataka kuwa na dhehebu lililo kubwa kuliko yote, wanataka kupata . . . Naam. La, wao ni—wao ni—wao ni, hawatawaambia hao wanawake hilo; hawatawaambia wanaume hilo; wanaogopa, maana hao wanatoa sadaka kubwa." Jinsi ambavyo hapana shaka ataona haya, Roho Mtakatifu, akiondoka kwa Mungu.

165 Aibu kwetu! Jinsi ambavyo hana budi kufanya hilo. Anawezaje kamwe kumpa huyo mwana chochote? Unajua kinachompata huyo mwana? Yeye daima ni mwana. Hakika, naam, bwana, bali yeye hana urithi.

166 Paulo alisema, "Nisije nikaihubiri Injili na mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa, mnaona." Naam. Yeye haufikii urithi, mnaona, mvulana huyo sikuzote ni mwana, bali yeye ni mwana mwasi tu.

167 Lakini vipi kama yule Mwalimu akija na kusema, "Hei, unajua nini? Mvulana huyo Wako ni, vema, mbona, yeye ni . . . " Kunradhi kwa hili tamshi; natumaini si la kukufuru kwenu. "Yeye ni mwana anayemshabihi sana mzee baba yake. Unajua nini? Yeye ni kama tu Wewe kabisa. Yeye hufanya jambo lile lile tu ulilofanya Wewe. Yeye . . . nitakwambia, anapoona lolote kasoro yeye husimama pale pale na kulitaja. Unaweza kumtumainia."

168 Jinsi, Baba hapana shaka atasema, "Naam, um-hum, huyo ni mwanangu. Huyo ni mwanangu." Ningali niko kwenye uzao wa Ibrahimu sasa. Sijauondokea huo; ninadumu na huo. "Huyo ni

mwana Wangu." Unajua kile Baba afanyacho baada ya mvulana huyo kuthibitishwa kwamba ni mvulana?

169 "Vema," wasema, "Biblia ilisema, *hili*, bali—bali hakika, sasa m—mzee wa jimbo atanifukuza kama nikihubiri *hilo*. Wao—wao—wao. . . Nikiwaambia wampokee Roho Mtakatifu bado. 'Loo, loo, loo, loo nisingekuwa na uhusiano wowote na hilo.' Lingefanya. . . Hao hawauamini huo."

"Vema, ninaamini katika utaka-. . . "

170 "Loo, la, la, la, la, la, la. Uponyaji wa Kiungu, sisi—sisi. . . Nitakwambia tutakalofanya. Tutavuta tu kundi fulani, nasi tutautupa nje upuuzi huu wote hapa wa uponyaji, na vurugu hii yote." Huh. Lakini Biblia ingali inaufundisha, ndugu. Hilo lingali ni Neno la Mungu. Kama wewe ni uzao wa Ibrahimu, utasimama na kila Neno lake. Hakuna kitu kitakachokukomesha. Hiyo ni kweli. Kama ni askofu wa Kimethodisti, ama mwangalizi wa Kibaptisti, ama baba wa Kipresbiteri, ama kasisi wa Katoliki, ama papa, ama yeyote yule. Hakuna kitu kitakachokukomesha endapo wewe ni uzao halisi wa Ibrahimu. Kweli. Dumu hapo. Naam, bwana. Hutoi msaada wako kutoka mfumo fulani wa kujibunia; unauvuta kutoka juu, kutoka kwa El-Shadai. Haleluya! Hiyo ni kweli. Lihubiri kwa vyovyote vile, na pasipo kujali linamwudhi nani. Lihubiri kwa vyovyote vile.

Baba alisema, "Hivyo ndivyo tu nilivyoliandika Neno Langu; hivyo ndivyo ninavyotaka lihubiriwe." Hiyo ni kweli.

171 Mnajua linalotukia? Basi, mnajua linalotukia? Wanafanya sherehe kwa ajili ya mwana huyo. Wanamtoa mwana huyo nje na kumvalisha vazi maalum (Mnajua hiyo ni kweli.), wanamweka mahali hadharani, na kufanya sherehe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka, na kumweka mwana huyo. Tangu wakati huo, jina la mwana huyo linafaa kwenye hundi kadiri la baba yake linavyofaa. Hiyo ni kweli?

172 Sasa, Mungu alifanya jambo lile lile na Mwana Wake. Yeye alimchukua Petro, Yakobo, na Yohana, wakapanda juu ya mlima. Ndipo wakati alipofanya jambo fulani kuu, Yeye aliwaita watatu kutoka Mbinguni: Musa, Eliya, na Kristo. Naye akatoa mashahidi watatu. Ndipo wakati wao waliposema, "Na tujenge vibanda vitatu hapa; tutakuwa na dhehebu liitwalo 'manabii'. Tutakuwa na moja lililoitiwa zile amri, Waadventista. Nasi tutaninii. . . " Kabla Petro hajamaliza kuongea. . . Wakati la kimbinguni linapotendwa, yeye anasisimkwa sana; anataka kuunda dhehebu.

173 Hapo ndipo ninyi ndugu wa Mvua ya Vuli mlipofanya kosa lenu. Hapo ndipo ninyi Waassemblies of God mlipofanya kosa lenu. Hapo ndipo ninyi wa Umoja mlipofanya kosa lenu. Hapo ndipo ninyi Church of God, Unabii, nanyi nyote, mlipofanya kosa lenu. Mliona ya kimbinguni yakifanywa; mlitaka kuchora

duara ndogo kuyazunguka na kusema, “Hii ni sisi.” Kwa nini msiachane nalo? Endapo si la Mungu, litakuwa ni bure. Na endapo ni la Mungu, mnawezaje kuling’oa; litasimama milele.

Songa mbele, elekeza jicho lako Kalvari, endelea kuvuta kutoka kwa El-Shadai. Hiyo ni kweli, dumu nalo.

174 Kutoa hoja na kujitenga: hivyo ndivyo ibilisi alivyosema, “Vema, ninaweza kuacha kupiga vita sasa; walielekezana bunduki. Almuradi wanapigana jinsi hiyo, niko sawa.” Mnaona? Anajilaza tu nyuma na kulala usingizi mdogo.

175 Lakini acha wao siku moja wakiondoe kitu hicho moyoni mwao na kurudi huku makwao, angalieni linalotukia basi. Hebu jeshi hilo kuu lisimame kwa mamilioni. Naam, bwana. Angalieni litakalotukia basi. Hebu Methodisti washushe bendera zao. Hebu Pentekoste washushe bendera zao. Hebu wote wawili wamshike Roho Mtakatifu na kusema, “Sisi hapa tumesimama.” Amina. Mtaona uamsho utakaotikisa taifa hili, hiyo ni kweli. Mtaona uamsho ambao nyinyi kamwe. . .

Unafikiri watafanya hivyo? La, bwana. Hawatafanya hivyo. Biblia inasema hawatafanya.

176 Billy Graham kote nchini; yeye alisema huko Louisville, nilipokuwa kwenye kiamshakinywa chake, yeye alisema, “Paulo aliingia mjini, akawa na mwongofu mmoja, akarudi katika—katika mwaka mwingine naye alikuwa na thelathini ama arobaini kutokana na huyo mmoja.” Kasema, “Ninaondoka na kupata elfu thelathini, narudi na siwezi kupata thelathini.” Jambo pekee ni kwamba, unawafanya wafanye maungamo ya macho makavu, Billy; wala huwaingizi kwenye kilindi vya kutosha katika Ufalme wa Mungu. Hiyo ndiyo shida. Hiyo ni kweli kabisa. Ila anaitumikia sehemu yake. Hebu kidogo; tutalifikia hilo, endapo mtanivumilia tu kidogo.

Angalieni. Yeye alimweka Mwana Wake; jambo lile lile alilomfanyia Ibrahimu. Alimwita Ibrahimu atoke.

177 Sasa, sikilizeni. Sasa, ninawatakeni mvae ufahamu wenu wa kiroho na kunyamaza kwa muda kidogo. Alimwita Ibrahimu atoke basi mwishoni mwa mlango huu wa 17, na, mlango wa 18, hasa, Yeye akamwita atoke na akamweka.

178 Akasema, “Abramu, mimi si. . .Jina lako si Abramu tena, bali jina lako ni Ibrahimu. Wewe si S-a-r-a-i, wewe ni *S-a-r-a* tangu sasa na kuendelea, ‘binti mfalme.’” Alifanya nini? Kumweka Mwanawe. Jina la Mungu ni nani? Elohimu. Hiyo ni kweli? Elohimu, hivyo ndivyo Yeye alivyo, Bwana Mungu Elohimu, Mhifadhi wa Mbinguni, mbingu na nchi?

179 Naye alimfanyia nini Ibrahimu? Alimpa Ibrahimu sehemu ya Jina Lake: kutoka kwa Abramu likawa Ibrahimu, Elohimu, kwa sababu yeye pia alikuwa ni baba (Amina.): akamweka,

mahali pake, akampa jina: Ibrahimu, kutoka kwa Abramu likawa Ibrahimu: Elohimu, Elohimu, h-e-i-m: h-a-m, Ibrahimu.

180 Ninawatakeni muone. Hiyo ilikuwa ni kabla tu ya yale maangamizi sasa na kabla ya kutimizwa kwa ile ahadi. Angalieni kwa muda kidogo tu sasa. Akiisha kumfanya hivyo, akaliweka jina lake sasa, akamweka mahali pake, akamwita kupitia kuhesabiwa haki (Mnaamini hilo?), uzao wake kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa kupitia kwa ile Damu, kupitia kwa ule uzao, kumjaza kwa Yeye Mwenyewe, kujimwaga Mwenyewe ndani yake kama El-Shadai, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu. Sasa, kumweka na kumpa sehemu ya Jina Lake, Elohimu, Elohimu mdogo, naye mwanadamu alizaliwa apate kuwa mungu mdogo.

181 Sasa, mnasema hilo ni kosa. Yesu alisema, "Hivi halininii . . . halisemi kwenye torati yenu wenyewe, 'Ninyi ni miungu'? Basi kwa nini mnanihukumu Mimi basi, kama torati yenu wenyewe inasema ninyi ni miungu." Yeye alipewa milki; milki hiyo ilikuwa ni dunia. Dunia nzima inaugua, ikingojea sasa madhihirisho ya wana wa Mungu.

182 Kama mimi ni Branham, mimi ni Branham; mimi ni sehemu ya Branham. Na endapo mtu ni mwana wa Mungu, Yeye amefanywa katika sura ya Mungu na kupewa milki hapa duniani kuitawala dunia hii kama Mungu alivyoitawala. Naye Adamu wa pili alilithibitisha. Amina. Yeye aliyakomesha maumbile: "Amani tulia." Amina. Aliulaani mtini, bila shaka, na Yeye alikuwa ni Mwanadamu hata hivyo alikuwa ni Mungu; Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa. Hivyo ndivyo tutakavyokuwa moja ya siku hizi. Tunalifikia tu kupitia kwa kuhesabiwa haki, wazao wa Ibrahimu wakija.

183 Sasa, angalieni kile alichomfanyia Ibrahimu: alimpa jina hilo. Sasa mara, yapata siku tatu ama nne baadaye, Ibrahimu alikuwa amejitenga na Lutu. Sasa, sikilizeni kwa makini sana sasa. Mko tayari? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa ninyi, mmelifuata kwa makini? Semeni, "Amina." ["Amina."] Mnaona mahali Yeye alipofanya kila kitu alichomfanyia Ibrahimu, Yeye ameufanyia uzao wake? Semeni, "Amina." ["Amina."] Sawa.

184 Sasa, tunashuka sasa kwenye jambo hilo jingine. Sasa, angalieni matabaka yetu matatu. Sasa, kulikuwa na . . . Neno *kanisa* linamaanisha nini? "Walioitwa watoke, walioitwa watoke." Israeli walikuwa ni watu wa Mungu mpaka walipoitwa kutoka Misri ndipo wakaitwa kanisa la Mungu. Mnaona? "Wakaitwa watoke," neno lenyewe, nenda ukaichukue kamusi yako uone kama si "kuitwa atoke."

185 Sasa, Ibrahimu alikuwa nini? Aliyeitwa na kutengwa. Yeye alikuwa Kanisa teule. Lutu analiwakilisha kanisa siku hizi. Tafadhali msilikose hili, tafadhali, katika Jina la Kristo

msilikose. Sikilizeni kwa makini. Kile yeye . . . Ibrahimu alikuwa hapa nje katika nchi ya uchovu, iliyochoka, isiyo na rutuba, hakuna maji kwa ajili ya ng'ombe, lakini Lutu alifanya nini? Yeye alikuwa ni Mkristo pia; alikuwa ni mwaminio. Kwa hiyo akashuka kwenda Sodoma na—na akawa meya wa huo mji. Hiyo ni kweli? Hayo ni madhehebu yenu, Mkristo wenu vuguvugu, anavyojiita. Huko chini hizo dhambi ziliitesa . . . Loo, kuwaona walevi kunaitesa roho yao. Hakika. Kulitesa moyo wao.

186 Sasa, kulikuwako na Wasodoma, wasioamini. Kulikuwako na Lutu papo hapo pamoja nao katika hali yake ya uvuguvugu, bali huyu hapa Ibrahimu. Loo, jamani. Kwa hiyo wakati unakaribia kwenye mwisho sasa. Basi angalieni kwa makini.

187 Siku moja wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi chini ya mwaloni wake, yeye aliwaona Watu watatu wakija wakitembea, mavumbi kwenye nguo Zao. Ndipo Ibrahimu akatoka nje, naye akasema, "Bwana wangu, hivi utaingia ndani? Kwa sababu hii umekuja." Jambo fulani lililokuwa moyoni mwa Ibrahimu, lilimfanya kuamini kuna jambo fulani pale kumhusu Mtu huyo.

Vema, Wao wakaingia. Sasa, sio "bwana zangu," Hao watatu; yeye alisema, "Bwana wangu."

188 Lutu, maskini yule aliyerudi nyuma, kasema, "Bwana zangu." Lakini Ibrahimu aliwaona Hao watatu na kusema, "Bwana wangu," Elohimu. Angalieni kama Biblia haisemi hivyo. Yeye alijua mahali alipokuwa. Yeye alikuwa uzao halisi wa Ibrahimu. "Bwana wangu, karibu. Ketini chini; nitawaletea maji kidogo; mnaweza kunawa miguu Yenu. Nami ni—nitawapa chakula kidogo, na ndipo mnaweza kuendelea na safari Yenu."

189 Yeye akaketi chini, na, nadhani, akachukua mgwisho. Ni wangapi wanaojua mgwisho ulikuwa ni nini? Jamani, loo, jamani, ni mara ngapi nimeutumia. Kwa hiyo akafanya hima akaenda kwenye kundi, akamshika ndama mdogo, mnono, akamchinja kisha akaja, kasema "Sara," huko nyuma kabisa hemani, "Nataka ukande mikate." Hiyo ni kuuchekecha. Ulipata kuona kichekecheo? Tulikuwa na kichekecheo cha kale duara; mama alikuwa na kabari ndani yake ambamo unga wa mahindi ungelowa maji na kunata. Angeusugua, maana ilikubidi kuwa mwangalifu sana kwake, mwajua. Basi sugua huu kabisa; yeye akasema, "Kanda kidogo ukaweke mekoni." Hawakuwa na karai ya mikate; walichukua tu meko pale, jiwe kuu lililowekwa huko nje mbele ya jiko, na kuuoka mkate huu upesi sana.

190 Kasema, "Nina hisia ndogo ya kwamba kuna Mtu fulani mgeni huko nje." Akaangalia huko nje, Hao walikuwa wamejaa mavumbi, Watu wa kawaida wameketi hapo nje chini ya kivuli cha mti, wakistarehe. Nao wakapika na kumwandaa huyo ndama, wa—wakatengeneza vipande vya nyama ya kondoo vizuri, na kupika ugali, kisha wakachukua siagi, na—na kisha wakachukua maziwa kutoka kwa ng'ombe; ndipo akaenda huko

nje akaketi, Nao wakala. Naye Ibrahimu akamwita Mtu huyo, "Elohimu": Mungu, akila nyama ya ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na akila ugali na siagi.

191 Sasa, endapo unataka kubishania hilo, ninii tu. . . Ibrahimu alizungumza na Yeye. Yeye alimwita "Elohimu," Bwana Mungu Mwenyezi. Ilikuwa ni kitu gani? Akionyesha yale uzao utakachopata. Angalieni sasa. Mungu. . .

192 Mhudumu fulani aliniambia wakati mmoja nilipozungumza juu ya hilo hapa siku chache zilizopita; akasema, "Kasisi Branham, wewe ni mtu mwenye akili sana kusema ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu."

Nikasema, "Basi ndivyo nilivyo, naam, mwenye akili kutosha kujua Biblia ilisema ilikuwa hivyo."

Naye akasema, "Unataka kusema ya kwamba Mungu alikuwa pale a—amevaa nguo nazo zina mavumbi, Yehova Mwenyezi?"

Nikasema, "Ibrahimu alimwita 'Elohimu.'"

Kasema, "Unafikiri hao wengine wawili walikuwa ni akina nani?"

Nikasema, "Malaika wawili."

Akasema, "Vema, una. . ."

Nikasema, "Mara Yeye alipokula hicho alitoweka." Nikasema, "Mbona, wewe hujui Mungu wetu ni Nani."

Nilikuwa, kama, nilikuwa nikichanua nywele zangu mbili ama tatu zilizosalia, mwajua, hivi majuzi, ndipo mke wangu akaniambia, kasema, "Billy, wewe karibu ni kipara."

Nikasema, "Sijapoteza hata mmoja."

Akasema, "Naomba uniambie mahali zilipo."

193 Nikasema, "Vema kipenzi, nitakwambia. Hebu niambie mahali zilipokuwa kabla sijazipata. Zilikuwa ni bayana. Na kokote zilikokuwa kabla sijazipata, ziko huko zikiningojea niziendee." Haleluya!

194 Huenda mwili huu usiwe kijiko kimoja cha mavumbi; hivyo ndivyo ulivyokuwa kwanza, wakati volkano ilipokuwa ikilipuka huko nyuma wakati mwili wangu ulipolazwa mle. Mungu yeye yule aliyenileta na kunilisha anaweza kuniinua juu tena, mahali fulani. Hiyo ni kweli.

Nikasema, "Tumefanywa kwa elementi kumi na sita za duniani: petroli, nurulimwengu, na kalisi, potashi."

195 Mungu alisema tu, "Nimesikia kuhusu dhambi huko Sodoma. Nitashuka chini nami itanibidi kutembea huko chini na kuangalia kote," na kusema, "*Phfff*," akaingia ndani yake, kasema. . . Akachota konzi jingine la kalisi, kasema, "*Phfff*, njoo hapa, Gabrieli. *Phfff*, njoo hapa, Mikaeli. Hima tushuke

chini." Hawa hapa wanakuja, wakishuka kuja. "Ninaenda kuwaonyesha yatakayotukia katika siku za mwisho kwa Uzao wa Ibrahimu kwa vyovyote vile." Sasa sikilizeni, kamwe msilikose hili.

196 Kwa hiyo basi Yeye anashuka karibu, anaketi chini, Nao wanaanza kuzungumza, na baada ya kula, mwajua, wawili wa Hao wakashuka kwenda Sodoma kulihubiri kanisa vuguvugu. Mlijua hilo? Walikuwa na uamsho huko chini. Basi si ni ajabu kwamba katika siku hii ya mwisho. . . Sasa, Mmoja Wao alibaki nyuma na kulizungumzia Kanisa teule, Ibrahimu na kundi lake teule. Ni wangapi wanaofahamu hilo sasa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nao hao wengine wakashuka na kuzungumza na Lutu wapate kumtoa Sodoma, kwa sababu yeye alikuwa mtu mwenye haki. Wote wanaoelewa hilo, semeni, "Amina." ["Amina."] Biblia inatufundisha ya kwamba Ibrahimu aliwakilisha Kanisa teule kama vile uzao wa Ibrahimu (Mnaona?), Ibrahimu aliyeamini, akijitenga mwenyewe. . . akimwamini Mungu, akijitenga na ulimwengu, akapitia kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kisha kuwekwa kwa karama, wana katika mwili. Sasa, yeye anangojea. Mnaona umbali tuliokuja?

197 Sasa, hapa yule Malaika anashuka katika mwili wa kibinadamu: Mungu, Elohimu. Inasema Elohimu, herufi kubwa B-w-a-n-a pale? Someni Mwanzo 18, mwone kama sivyo. Elohimu alishuka katika mwili wa mwanadamu, akala kama mwanadamu, akanywa maziwa kama mwanadamu, akala nyama ya ndama kama mwanadamu, akala siagi na ugali kama mwanadamu. Sasa, ukitaka kubishana, basi bishana na Yeye.

Angalieni yale yaliyotukia. Na kulikuwako na Mmoja aliyebaki nyuma kwa Ibrahimu, na hao wengine wakashuka kuhubiri kwa kanisa vuguvugu, Billy Graham wa kisasa.

198 Mliona ni ajabu jinsi gani katika siku hizi za mwisho, jinsi ambavyo A-b-e-r-h-a-m, ambaye agano lilifanywa naye, na mtu mmoja katika agano lake akilihubiria kanisa vuguvugu: G-r-a-h-a-m? Mliwahi kuwazia jinsi hilo lilivyokuwa ni la kigeni? Sio Billy Sunday, bali (Mnaona?) G-r-a-h-a-m, yule mjumbe kwa kanisa vuguvugu kuwaita watoke Sodoma. Na Mmoja alibaki huko nyuma pamoja na Ibrahimu.

199 Angalieni vile yu—yule aliyeshuka na kuhubiri. Alifanya nini? Alipiga makelele, "Ondokeni kwake." Alifanya nini? Sio miujiza mingi, haikufanywa kwa wingi. Ila tu aliyapofusha macho yao. Nako kuhubiriwa kwa Injili huyapofusha macho ya asiyeamini. Ilikuwa ni kitu gani? Aliyapofusha macho yao kusudi wasiuone mlango. Hiyo ndiyo shida sasa. Hawaujui Mlango, Mlango ni Yesu, Roho Mtakatifu aliye hai kwa Kanisa. Amina. Akahubiri vema, bali akawapofusha wasiuone mlango huo.

“Siku za miujiza zimepita, bali Yeye angali ni Mungu.” Na kadhalika.

“Ondokeni hapa, maana nitapateketeza.” Hiyo ni kweli.

Hebu mwangalieni Yule aliyebaki pamoja na Ibrahimu; Yeye alitoa—Yeye alitoa ishara huko nyuma, pia. Ee Mungu!

200 Wanawake siku hizo hawakuwa kama walivyo siku hizi; kila wakati mtu fulani anapokuja, mwanamume fulani, inawabidi kuvaa kaptura zao na kukimbia nje, wakakate nyasi, na, mwajua, kushughulikia kazi za mumewe, na kila kitu. Walikaa nyuma hemani mahali pao. Kama wangewaondoa wanawake wote ofisini huku, pamoja na waume na wote, kutembea... kufanya kazi, na kuwaweka mahali pao, na kuwaondoa hawa polisi wanawake barabarani, fedheha kwa hii...doa kwenye bendera, na kuwarudisha, wanaume wangepata kazi.

201 Malaika akaketi na kuanza kuzungumza na Ibrahimu, kasema, “Nadhani unajua ni kwa nini nimeshuka.” Sasa, angalieni. Yeye hakusema, “Abramu.” Alisema, “Ibrahimu.” Mbona, siku chache tu kabla ya hapo alikuwa Abramu. “Ibrahimu, yu wapi mkeo Sara?” S-a-r-a. Angalieni kama hiyo ni kweli. Yapata siku mbili tu kabla ya hapo alikuwa tu amepewa jina hilo. Yeye alijuaje jina lake lilikuwa Ibrahimu, alijuaje jina la mkewe lilikuwa Sara. Mnaona, yeye hakuwa amekimbia nje na kuingilia kazi ya mume wake. Kwa hiyo, mnaona?

Ibrahimu (Sasa sikilizeni, Biblia, ninainukuu Biblia.) kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.” Hiyo ni kweli? Sasa, angalieni.

202 “Ibrahimu, nitakuzuru kulingana na ahadi Yangu.” Ilikuwa ni nani? Ilikuwa ni nani? Si ajabu Ibrahimu alimwita Elohimu. “Nitaifanya ahadi Yangu itimie.”

203 Naye Sara...Samahani, enyi wasichana, Sara huko nyuma hemani, mwanamke wa kupendeza, bali yeye alisema, “Mimi, mwanamke mkongwe, karibu umri wa miaka mia moja, naye bwana wangu...” (mumewe) “...mia moja pia, ati nipate raha naye tena?” Mnaelewa ninalomaanisha, sivyo? Kama mume na mke ilikuwa imekoma. Mnaona? Kasema, “Nipate raha kama msichana tena pamoja na mume wa—wangu huko nje?” Wakati huenda hiyo ilikuwa ni miaka ishirini iliyopita hapo kabla, uhusiano kama huo wa kifamilia. Mnaona? “Mimi, mwanamke mkongwe nipate raha na mume wangu, naye ni mkongwe pia?” Akasema, “Ha-ha.”

204 Ndipo Malaika huyu, Elohimu katika mwili, akamwangalia Ibrahimu na kusema, “Mbona Sara akacheka, akisema moyoni mwake mambo haya yasingewezekana?” Mnaona ni ishara ya jinsi gani Kanisa teule lilipata? Mnaona ni ishara ya namna gani Billy Graham anayotoa? Angalieni ilivyo hapa katika Kanisa teule. Ni Mungu ndani ya mwili wako, akijidhihirisha. Basi Yesu hakusema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo

itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu?" Mnaiona sasa? Sasa, tumepita kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuwekwa kwa karama za Mwana Kanisani. Sasa, ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kwa ajili ya ishara hiyo. Basi namwomba msomaji yeyote wa Biblia anionyeshe ishara moja zaidi aliyofanya Yeye kabla . . . baada ya hayo.

Sasa. Sasa, hebu—hebu tupige hatua ndogo mbele kidogo. Yeye alisema, "Yuko hemani nyuma Yako."

205 Sasa angalieni, Mungu angalimhukumu mwanamke huyo papo hapo kwa kutomwamini Malaika huyo. Mnaamini hilo? Ila asingeweza kufanya hivyo. Na jinsi baadhi yenu Wapentekoste, sisi Wapentekoste tunavyotenda, tungalitupwa nje muda mrefu uliopita; bali Mungu hawezi kufanya hivyo. Kwa nini? Kama angalimtupa nje I-. . ., ama, kama angalimtupa nje Sara, yeye alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Kwa hiyo alikuwa mrithi pamoja naye. Kwa hiyo ingemlazimu kumtupa nje Ibrahimu pia, kwa hiyo asingeweza kufanya hivyo kwa ajili ya mke wake, kwa ajili ya mumewe.

206 Kwa hiyo hiyo ndiyo njia, ni kwa sababu ya Kristo Yeye hawezi kututupa nje. Sisi ni wana na binti Zake. Kutokuamini kwetu hakumaanishi lolote. Uzao halisi wa kweli wa Ibrahimu utanawiri kwa vyovyote vile. Hilo hapo.

207 Sikilizeni kwa makini sasa. Ndipo Malaika akasema, "Nitakuzuru; kulingana, wakati wa uhai, mbona, jambo hili litatukia." Ndipo Ibrahimu akaambatana Naye, Naye akatoweka na kwenda zake; huko gizani mahali fulani akaenda, akageuka kuwa Mungu tena.

208 Tumeona kuhesabiwa haki? tumeona kutakaswa? ubatizo wa Roho Mtakatifu? kuingia katika Mwili wa Mungu? Tumeona kuwekwa kwa karama Kanisani? Sasa tumeona kudhihirishwa kwa Mungu, ile ishara ya mwisho?

Sasa, angalieni. Mara Mungu akafanya jambo fulani kwa Sara na Ibrahimu. Sasa, hamtaamini *hili*, bali *ndivyo* ilivyo kwa vyovyote vile.

209 Mnaona, kile . . . ukitaka kuisoma Biblia, huisomi kama tu vile unavyosoma gazetini, "Nao walikuwa na mlipuko hivi majuzi." Sasa, sijui kama ni kweli ama si kweli. Wanatwambia mambo mengi sana ya uongo, kamwe huwezi kuvutiwa nayo. Lakini unapoisoma Biblia, ni Barua ya upendo kwa Kanisa.

Biblia ilisema ya kwamba Yesu alimshukuru Mungu kwa kuyaficha macho ya wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga, ambao wangeweza kujifunza.

210 Ninapoenda kwenye nchi za ng'ambo, maskini mke wangu mpendwa ataniandikia barua: "Mpendwa Billy, nimeketi hapa usiku wa leo pamoja na watoto. Ndio kwanza tuwalaze kitandani." Mimi . . . "Mtoto Joseph alilia kidogo usiku wa leo

kwa ajili yako kabla hajaenda kulala." Ninajua kile anacho— kile anachoandika. Lakini ninampenda sana, ninaweza kusoma katikati ya mistari; ninajua kile anachozungumzia.

211 Hivyo ndivyo inavyokupasa kulisoma Neno la Mungu: katikati ya mistari. Kama unampenda, Yeye anakufunulia tu. Unaanzia hapo, nawe unaninii tu, "Mbona, linasema, 'Hili hapa.'" Mbona, unasema, "Hili hapa." Hakika.

Sasa angalieni, mnajua kile Yeye alichowafanyia Sara na Ibrahimu? Sasa sikilizeni kwa utulivu sana. Aliwabadilisha wakawa kijana mwanamume na mwanamke.

"Ninataka uthibitishe kwamba Yeye alifanya hivyo."

212 Sasa, sikilizeni kwa makini. Jambo la kwanza, mnajua mara moja Ibrahimu na Sara waliondoka kwenye nchi hiyo na kuhamia Gerari. Hiyo ni kweli? Ipime kwenye ramani; ni mbali sana kwa mtu mkongwe, maskini nyanya aliyevaa kijikofia kidogo kichwani mwake, mwajua.

Sasa, mnasema, "Loo, vema, waliishi tu muda mrefu zaidi."

Biblia ilisema, "Walikuwa na umri mkubwa, na wamepita wakati wa kuishi maisha ya binadamu." Maskini bikizee, huyu hapa anaenda.

213 Wakafika kule chini, na walipowasili kule chini, kulikuwako na m—mfalme kijana huko chini jina lake Abimeleki aliyekuwa akijitafutia kipenzi. Na wasichana wote warembo wa Kifilisti wakiwa huko, wakati alipomwona huyu bikizee akija, yeye alisema, "Huyo ndiye wangu." Akampenda na kusema, "Unaonekana mrembo."

214 Aibu kwenu. Maskini bikizee hata asingeweza kuishi na mume wake mwenyewe, hakuwa ameishi naye kwa miaka kadhaa, kisha akamdhihaki Malaika hata kwa kusema angefanya hivyo. Yeye alimfanya msichana. Alikuwa mzuri na mrembo.

215 Sasa angalieni, hebu niwaambie jambo fulani. Ingemlazimu kuninii. . . Yeye alimfanyia jambo fulani. Sasa, vipi kama Yeye angemrutubisha tu? Vipi kama angeninii tu. . . Kama angalifanya hivyo. . . Hawakuvuta sigara siku hizo na kuwalazimu kuwalea watoto wao kwa chupa. Mnaona? Hawakuwa nayo. Iliwabidi kuwalea kwa matiti. Mishipa ya maziwa ilikuwa imekauka. Mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja akipata utungu wa kuzaa, angekufa katika dakika moja, hakika angekufa. Ilimbidi kumpa moyo mpya; ilimbidi kumpa mishipa ya maziwa; ilimbidi kurutubisha tumbo lake la uzazi; ilimbidi kuninii. . .

216 Loo, angalia kile kilichombidi kumfanyia Ibrahimu, mwili wake ukiwa kama uliokufa. Yeye alimbadilisha tu tena. Maana anaonyesha kile atakachoufanyia uzao wa Ibrahimu. Mnaona?

217 Angalieni. Yeye aliendа huko chini, na kwa hiyo Abimeleki akampenda. Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Naye akamchukua kama mkewe. Naye alikuwa akitaka kumkaribia kwa sababu alikuwa ni msichana mrembo. Ndipo usiku huo huyo ndugu mzuri wa kisheria alikuwa amelala huko, mwajua. Akafanya sala zake, kisha akaoga mwili, na kunyosha vidole vyake vya miguu juu. Kesho atamwoa msichana huyu mrembo wa Kiebrania; jamani, mwenye umri wa miaka mia moja tu. Mnaona? Na loo, jinsi. . .mara. . .jinsi alivyokuwa ni mrembo. Naye mumewe kijana ameketi kule nje.

218 Basi usiku huo Bwana akamtokea katika ndoto na kusema, "Wewe ni kama mtu aliyekufa." Hiyo ni kweli. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani, kama ninyi nyote mko—mko sawa kwa ajili ya uponyaji wenu jioni ya leo ama la.

Mbona, akasema, "Bwana, Wewe unajua unyofu wa moyo wangu." Kasema, "Mwanamke huyo aliniambia ya kwamba huyo alikuwa ni ndugu yake."

219 Kasema, "Huyo ni mke wa mtu." Sikilizeni, hii hapa ile sehemu: Kasema, "Mume wake ni nabii Wangu. Na sijali utaomba kiasi gani; kamwe sitakusikia. Nenda, acha akuombee, ndipo nitakuponya."

220 Ameketi pale akisema uongo, na mwanamume ambaye angesema hivyo dhidi ya mkewe kuiokoa shingo yake; ninyi ni wastahilifu hivyo? Mnaona? Ninajaribu kufanya nini? Kuwaonyesha ya kwamba ni neema ya Mungu iliyowafanya wastahilifu. Hufai kitu; mimi sifai kitu; bali Yeye Ndiye aliye mwema. Mtazameni Yeye. Yeye Ndiye aliyelifanya. Isingalikuwa ni kwa neema ya Mungu; Ibrahimu aliketi pale, akadanganya. Alikuwa akidanganya? Alifanya hivyo? Alisema, "Huyo ni dada yangu." Ni maskini uongo usiodhuru: ni makubwa meusi.

Naye akasema, "Huyo ni ndugu yangu." Na hilo lilikuwa ni kosa. Ila analisema kwa njia ya mzunguko apate kuokoa shingo yake.

221 Ndipo Yeye akasema, "Nenda huko nje na kuombea. . . umwache akuombee." Ndipo Ibrahimu akamwombea, akayarejesha maisha yake, na nini? Baadaye, wakampata huyo mtoto.

222 Ninataka muone. Katika kufunga sina budi kusema jambo hili. Siwezi kuyafikia hayo mengine; tumechelewa mno, kisha tufanye mstari wa maombi. Ninataka kusema jambo hili: Yeye alimfanyia nini Ibrahimu? Kuhesabiwa haki wakati alipoamini. Hiyo ni kweli? Semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kutakaswa wakati Yeye. . .kwa damu. Hiyo ni kweli? Ibrahimu na uzao wake. . .Akampa nguvu kutoka kwa mwili Wake Mwenyewe, jambo lile lile wakati Yeye anapompa Roho Mtakatifu, nguvu kutoka katika Utu Wake Mwenyewe. Hiyo ni kweli? Akamweka kama wana katika

mwili—katika mwili pamoja na karama; hiyo ni kweli? Na sasa anajidhihirisha Mwenyewe kama Yehova; akishuhudiwa na Yesu Kristo, kujua siri za moyo kama tu Yesu alivyosema.

223 Kumbukeni, Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye aliwathibitishia Wayahudi alikuwa ni Masihi kwa ishara hiyo. Hiyo ni kweli? Alilithibitisha kwa Wasamaria; walikuwa wakimtazamia Masihi. Hiyo ni kweli? Lakini hakuna mahali kwa Mataifa, hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Tunamtazamia Masihi, sivyo? Kwa hiyo sasa analithibitisha kwetu sasa.

224 Basi angalieni, Yeye alifanya nini? Ilimbidi kuubadilisha mwili wa Ibrahimu na wa Sara. Lilikuwa ndilo jambo lililofuata baada ya ishara hiyo kuonyeshwa kwamba Yeye alijua siri za moyo wao, Yeye alibadilisha. . .Jambo la pili lilikuwa ni kubadilishwa mwili kusudi apate kumpokea mwana aliyeahidiwa. Basi hilo ndilo jambo linalofuata sasa ni ule Unyakuo wa Kanisa, kule kubadilishwa. "Sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia wale waliokwisha kulala mauti; kwa maana parapanda ya Mungu italia; waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza, kisha sisi tulio hai tutabadilishwa katika kufumba na kufumbua jicho."

225 Basi angalieni, vipi kama Yeye aliwabadilisha tu kuwa kijana mwanamume na mwanamke kama walivyokuwa hapo mwanzo? Wasingaliweza kumpata huyo mtoto kwa vyovyote vile, kwa sababu walikuwa wameishi pamoja wakati wakiwa kijana mwanamume na mwanamke. Ilimbidi kuubadilisha mwili wao kwa njia tofauti kusudi waweze kumpokea mwa-. . . kumpata mwana. Hiyo ni kweli? Ilibidi mwili wao ubadilishwe kwa njia nyingine, wapate kumpokea mwana.

226 Nasi hatuwezi. . .Kama tungerudi kuwa vijana wanaume na wanawake, bado hatuwezi kumlaki yule Mwana, kwa sababu tutamlaki hewani. Inatupasa kuwa na mwili uliobadilishwa kumlaki hewani, ule Unyakuo.

227 Hilo ndilo jambo linalofuata kwa ajili ya watoto wa Ibrahimu. Parapanda italia jambo la pili. Watoto halisi wa Ibrahimu watabadilishwa, mwili huu utafanywa mwepesi nasi tutapaa moja kwa moja juu. Kama tukirudi kuwa vijana wanaume na wanawake, tungali tungekuwa wasioweza kuondoka duniani. Kama Ibrahimu na Sara walirudi kuwa kijana mwanamume na mwanamke, wasingeweza kumzaa huyo mtoto, maana walikuwa wangali tasa. Lakini Yeye aliwabadilisha kusudi wapate kumpokea mwana aliyeahidiwa, na kama Yeye alivyomfanyia Ibrahimu. . .Angalia jinsi Yeye alivyoshusha kila kitu kupitia kwa Ibrahimu, kila kitu kupitia uzao wa Ibrahimu, nasi hapa papa hapa leo hii tukingojea Kunyakuliwa mara moja, mara baada ya hilo kunakuja kule kubadilishwa na yule mwana.

228 Hivi tunamtazamia Mwana? Tunamtazamia Mwana wa aina gani? Mwana wa Mungu akizuka akiwa na uponyaji katika mbawa Zake. Haleluya! Ibrahimu na uzao wake baada yake, sasa mnaelewa? Mnaona ni kwa nini nina shauku sana?

229 Nina yapata Maandiko kumi ama kumi na mawili zaidi hapa ninayopaswa kuyafikia, bali hatuna wakati. Ninawatakeni mwe na kanisa lenu usiku wa leo. Ningepaswa kuwa nikienda zangu nyumbani dakika ishirini ama thelathini zilizopita.

230 Lakini mnaona ninalomaanisha? Yale aliyomfanyia Ibrahimu, Yeye aliufanyia uzao wake. Hiyo ni kweli? Uzao ulikuwa ni nini? Mataifa wakati haikuwa tu ni watu. Mungu huwashughulikia Israeli kama . . .

Huyu hapa mtu ameketi papa hapa, aliyenijia hivi majuzi, na kusema, "Ninajaribu kujiandaa kuwa mmishenari kwa Wayahudi."

231 Nikasema, "Sahau hilo. Maskini Wayahudi hawa waliotawanyika, sio Wayahudi ambao Mungu anazungumza habari zao. Mungu huwashughulikia Wayahudi, sio kama mtu binafsi, bali taifa." Israeli iko tayari kumpokea Roho wakati Eliya na Musa watakapowatokea baada ya Unyakuo wa Kanisa. Jambo lifuatalo ni mtini ukichanua maua yake. Hao ndio wa kweli. Kwa hiyo wanakuja kwenye nchi ya uenyeji wao; bali Israeli itapokelewa kama taifa. Sisi ni kama watu binafsi, uzao wa Ibrahimu. Kwa hiyo sasa, sisi . . . Huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu. Nanyi liandikeni tu, enyi vijana, katika Kitabu chenu, mwone jinsi—jinsi . . . kama hiyo ni kweli ama si kweli. Mnaona?

232 Lakini sasa, kanisa la Mataifa limekwisha. Kunaye Billy G-r-a-h-a-m huko Sodoma, akiwavuta hao Wasodoma kwa nguvu awezavyo. Malaika wa Bwana hapa miongoni mwa Kanisa teule ambalo limeitwa litoke, linaloitwa "watakatifu wanaojibingirisha" kama vile Ibrahimu, "Wenye kichaa, kwa nini msishuke mje mkashirikiane na kujifurahisha na wengine wetu; tunaishi hapa katika anasa," na mambo kama hayo. Lakini kuna uzao wa kweli wa Ibrahimu ambao hawaugusi ulimwengu wala mambo ya ulimwengu. Ni kitu gani? Ni ujumbe gani unaoendelea?

233 Mtu mmoja alikutana nami hivi majuzi usiku na kusema, "Ndugu Branham, kama utapatana tu . . . " Mtu mashuhuri wa kanisa la Full Gospel kasema, "Tutakuchukua na kukupatia ndege kama utajiunga na dhehebu letu, nasi tutakuchukua pamoja na karama hii kwenye kila mji mkuu ulimwenguni na kukitangaza kitu hiki kote, endapo utapatana tu kidogo juu ya yale unayofundisha."

234 Nikasema, "Wewe, pamoja na digrii yako ya uzamili unamwomba mtumishi wa Mungu kupatana juu ya Neno la Mungu. Siwezi kuwazia jambo kama hilo, jamani." Nikasema,

"La, bwana kamwe sitapatana hata kidogo." Nikasema, "Ninaamini Neno la Mungu linafundisha Kuja kwa Mwana wa Mungu. Ninaamini katika Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninaamini katika ishara na maajabu kuwafuata waaminio. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema hasa. Hayo ndiyo ninayotetea. Hayo ndiyo ninayoamini." Nami najua hilo ni kweli.

235 Nasi tumepitia kwenye kuhesabiwa haki kwa Martin Luther kama vile Ibrahimu alivyofanya; tumepitia kwenye utakaso wa Wesley; tumepitia kwenye wakati wa Kipentekoste; na sasa tumeona kule kuwekwa kwa karama kanisani. Na sasa ni kitu gani tunachoona tena? Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mwili, akiyatambua mawazo hasa ya moyo, vile hasa Yesu alivyosema ingetimia. Basi jambo linalofuata ni kule kubadilishwa kwa mwili kumpokea Mwana aliyeahidiwa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

236 Baba wa Mbinguni, sijui lingine lolote la kusema kwenye saa hii. Hakika watu wanaweza kufahamu, Bwana. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Sayansi inasema kwamba tuko, miaka mitatu ama minne iliyopita tuko kwenye usiku wa manane kasoro dakika mbili, ama, dakika tatu. Ninaamini ya kwamba mkono mkuu wa Mungu ulinyoshwa ukausimamisha wakati. Kile kifuniko cha piramidi kiko karibu kuwekwa juu. Kanisa linachongwa, linaiona ishara yake ya mwisho.

237 Bwana, jalia watu hao waamke na kutambua wanatazamia jambo fulani huko mbali sana usoni, nalo linatukia moja kwa moja chini ya pua yao, wala hawatambui. Kama ibilisi anaweza kuwafanya waamini jambo hilo, Bwana, yeye—yeye amewashinda kabisa. Jalia watambue, Bwana, ya kwamba huyu—huyu Roho Mtakatifu tunayemfurahia, na tumekuwa tukimfurahia kwa miaka hii yote, ni Wewe. Ni Kristo, lile Agano ambalo Mungu alifanya na jamiii ya wanadamu, tupate kuwa wana na binti, kama Roho Wake aliishi ndani yetu. Nasi tungefanya jambo lile lile.

238 Elohimu yule kule chini alikuwa ni nani? Mbona, ilikuwa ni Wewe, Yesu, Yule mpakwa mafuta aliyeupaka mafuta mwili wa nyama kuonyesha ya kwamba katika siku za mwisho Wewe ungejidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu. Nasi tunakuona Wewe ukifanya hivyo kila mchana na usiku. Na hili limekuwa likiendelea sasa kwa mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili, na sisi hapa.

239 Tumepitia kwenye wakati wa Luther, kama vile ulivyomchukua Ibrahimu, tukapitia kwenye wakati wa Wesley, kama ulivyomfanya Ibrahimu, tukapitia wakati wa Pentekoste: likajifanyia utaratibu na kujiundia dhehebu na kurudishwa kwenye rafu. Kanisa likisonga mbele moja kwa moja, moja kwa moja; maskini itikadi ndogo zikijaribu kuibuka, lakini kila

mmea ambao Baba yangu hakupanda utang'olewa, unakufa papo hapo.

240 Lakini sisi hapa sasa kumwona Mungu akiishi miongoni mwetu, akijionyesha Mwenyewe. Tunangojea hata kwenye ule Unyakuo, kule kubadilishwa tupate kumwona Mwana wa Mungu akija katika utukufu moja ya siku hizi. Yeye kamwe hataigusa dunia kwa miguu Yake, bali sisi tutabadilishwa na kunyakuliwa kumlaki Yeye hewani. Kama vile ulivyombadilisha Sara na Ibrahimu, na kuwafanya katika hali ambapo wangeweza kuona, na kumpokea mwana aliyeahidiwa ambaye walikuwa wamemngojea, Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utaibadilisha miili yetu ipatikanayo na mauti moja ya siku hizi. Kama vile lile ono, ama kuhamishwa, ama chochote kilichokuwa hivi majuzi usiku, tutanyakuliwa moja ya siku hizi, tutabadilishwa, ninii tu . . . Bwana, ninaliamini kwa yote yaliyo moyoni mwangu. Wazee watakuwa vijana, nguvu za Mungu zitaninii . . .

241 Moja ya siku hizi tutakuwa tumeketi mkutanoni, wengine huko nje mashambani, wengine wakisaga kwenye kinu, ndipo mara kutakuwako na kelele kutoka Mbinguni. "Tazameni Bwana-arusi yuaja." Ndipo tukisimama pale huku mikono yetu ikiwa hewani, na kujua ya kwamba sisi ni wana wa Mungu na warithi pamoja na Ibrahimu kupitia Yesu Kristo, yule Mzao wa Kifalme, kujua ya kwamba ishara zile zile zilizofanywa kule kwa Ibrahimu, tunaziona zikifanywa siku hizi na zilizoahidiwa na Yesu Kristo, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma, ndivyo itakavyokuwa."

242 Kabla ya Sodoma kuteketezwa, ulimwengu kuteketezwa tena, na kabla ya kuteketezwa mara ya pili, jambo lile lile litatukia tena.

243 Nasi tunamwona Billy Graham huko chini Sodoma, akiihubiri Injili kwa kundi hilo la wasomi, akijaribu kuwaita watoke. Bibi Lutu pamoja na karamu zake zote, na wapendwa wake, wala hakutaka kutoka. Nasi tunaona wanawake wa kisasa waliovaa kaptura, na rangi, na kukata nywele, na kama Wasodoma; wakivalia kama makahaba, kutamanisha kijinsia, kusudi wanaume waweze kuwaangalia, kisha wawe na hatia ya kufanya uzinzi pamoja na mwanamume huyo, ingawa ni safi mwilini mwao; lakini, "Kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye." Amezini naye, yeye atawajibika kwa ajili yake. Tunamwona Bibi Lutu akifanya jambo lile lile.

244 Mungu, jinsi ambavyo tungeweza kudumu na hili hadi asubuhi, na kesho usiku, na asubuhi inayofuata, kuendelea na kuendelea: Jinsi huyo mwana alivyokuja na jinsi alivyotolewa dhabihu; jinsi ambavyo yule kondoo dume alikuwa juu ya mlima. Si ono, bali kondoo dume ambaye Mungu alimwagiza Ibrahimu

kumchinja badala ya mwanawe, na damu ikamtoka; na damu haitiririki kutoka kwenye ono. Ilikuwa ni kondoo dume; Yehova-yire.

245 Mungu, Wewe unaweza alasiri ya leo kujitolea Mwenyewe Dhabihu. Unaweza kujitolea Mwenyewe Kanisa; unaweza kujitolea wahudumu ambao watainuka na kuihubiri kweli, bila kujali yale shirika, madhehebu, na maaskofu, na mapapa, na kadhalika wasemayo. Wewe ni Yehova-yire. Ninakupenda, Bwana. Ninakupenda.

246 Nami nalikabidhi kusanyiko hili Kwako. Ninawakabidhi ndugu zangu wapendwa hapa, wanaoiamini Injili ii hii. Mungu, naomba ya kwamba Wewe utawafanya watu wenye nguvu wa Mungu, Ee Mungu, watakaookaa kwenye mstari wa kuchongea, Injili, sio kupatana kwa chochote, haidhuru itawagharimu nini. Ninaomba ya kwamba Wewe utafawafanyia watu hawa wa ajabu humu ndani alasiri ya leo jambo lile lile.

247 Sasa, Bwana, nimelihubiri Neno kwa udhahiri nilijuavyo. Nimewaonyesha kwa mifano katika mfano wa kitoto hata mtu yeyote angeweza kuelewa. Sasa, Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Elohimu, Wewe ungali ni Elohimu. Ninaomba ya kwamba utamleta Roho Wako humu miongoni mwetu alasiri ya leo, na kwamba nguvu Zako kuu zitakuja na kutuonyesha ile ishara inayoonekana kabisa uliyomwonyesha Ibrahimu na Sara kabla ule wakati haujatimia. Tujalie, Bwana. Kanisa hili, nitakapoondoka alasiri ya leo, Ee wa Milele na Mbarikiwa, wapate kujua ya kwamba Wewe ni Yehova. Tujalie, Bwana, tujalie, naomba katika Jina la Yesu.

248 [Mtu fulani ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Mtu fulani anafasiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Roho Mtakatifu akisema ujumbe huo kwamba kama vile Yeye alivyokuwa pamoja na Ibrahimu na uzao wake, Yeye yupo hapa, uzao wa Ibrahimu, leo hii.

Iweni na kicho mbele za Mwenyezi Mungu. Nitawaomba kama . . . Unaweza kuinua kichwa chako. Ninawaomba mwe na kicho.

249 Nimepiga simu leo hii kwamba tutawaombea wagonjwa kuwaleta wagonjwa huku juu wala sitaki kuacha hili . . . kuacha fikra hii juu ya watu hawa hapa, ya kwamba kwa sababu nipo hapa, mimi ndimi ninayepaswa kuwaombea wagonjwa.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . huyo mwanamke mweusi. Naye anaombea shinikizo kuu la damu. Yeye . . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kutoka hapa; ametoka Chicago.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . juu, Bibi Jones.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Bibi Nola Jones, waweza kusimama? Amesimama?

250 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mmoja kwa mwingine, weka ninii wako. . .punga mkono wako namna hii, ili watu wajue ya kwamba mimi na wewe hatufahamiani. Nenda nyumbani. Yesu Kristo alikuponya.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mwanamke mwingine [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .?. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .roshani [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] zile nguvu za kutenda kazi, mvuto unatoka upande huu. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .?. . .mwenye ugonjwa wa koo. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .ana matatizo ya utumbo mpana. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .?. . .simama, na umwamini Bwana Yesu Kristo.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .huyo mama aliyeketi mwishoni kwenye safu hiyo hapo. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .shida unaamini Mungu atakuponya, mama?

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .sawa nenda zako nyumbani; Yesu Kristo anakuponya.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mwamini Mungu. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .Maskini mama huyo anayeketi papo hapo, kidogo ana moja ndefu inayoonekana ya waridi.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .kwa macho yake. Unaamini Mungu atakuponya?. . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .baridi yabisi, anasumbuliwa nayo, unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kuupokea pia.

251 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mwanamume anayeketi upande ule mwingine akiniangalia akiwa na ugonjwa huo wa uvimbe puani. Unaamini kwamba Mungu atakuponya, bwana? ugonjwa wa uvimbe puani? Vema bwana. Unayefuata una ugonjwa wa tumbo. Unaamini kwa moyo wako wote Mungu atakuponya? Una ugonjwa wa moyo wewe unayefuata. Unaamini Mungu atakuponya, mama? Unaamini? Unayemfuata, una yabisi kavu. Unaamini Mungu atakuponya? Vema bwana unaweza kuupokea. Nenda nyumbani ukaponywe.

252 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .Mungu atakuponya? Huko juu kwenye safu ya mwisho? Vema bwana, unaweza kuupokea. Aliye karibu nawe ana ugonjwa wa utumbo. Unafikiri Mungu atakuponya? Nenda ukaupokee.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .moyo wako wote? Mwamini Mungu.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . Uvimbe kwenye titi, Bi. Cramer, simama kwa miguu yako na ukaponywe.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . uzao baada Yake. Mungu aliahidi ya kwamba ingekuwa hivi katika siku za mwisho, enyi watoto. Mnaamini hilo?

Sasa, BWANA ASEMA HIVI . . .

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . Neno la Mungu linalithibitisha kwamba ni kweli. Nyote mnakuwa kama maziwa na kila mahali sasa kila kitu kinatendeka.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . hapa kutoka St. Louis.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . macho.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . . hapa ana pumu, iwapo unaamini unaweza kurudi ukaponywe.

253 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Neno limesema hivyo, Biblia imelitangaza kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Roho Mtakatifu alishuka, akaliweka kanisa Lake, akaliokoa, akalihesabia haki, akalitakasa, akalijaza kwa Uwepo Wake na sasa Wewe uko hapa katika kanisa Lako ukijionyesha Mwenyewe hai pamoja na watu Wako kabla tu ya Unyakuo; kule kubadilishwa kwa mwili.

61-0416 Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org